UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

# TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA UKWASI (LIQUID FUND)

UKWASI FUND
Uhuru kwa mwekezaji

## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2023

# YALIYOMO

1. Ratiba na Ajenda za Mkutano....ii
2. Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Nne....1
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Nne....24
4. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi....27
5. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko wa Ukwasi....30
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko....32
7. Taarifa ya Hesabu za Mfuko....35
8. Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji....40
9. Jarida la Habari....47

**KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS**
**MKUTANO MKUU WA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA UKWASI SIKU YA JUMAPILI, TAREHE 19 NOVEMBA 2023 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE – DAR ES SALAAM**

# RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO

| MTIRIRIKO WA SHUGHULI | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **MUDA** | **SHUGHULI** | **WAHUSIKA** |
| 1. | 02.30 - 02.45 | Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha | Wajumbe/Utawala |
| 2. | 02.45 - 03.00 | Matangazo na Shughuli za Utawala | MC/Utawala |
| 3. | 03.00 - 03.05 | Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |
| 4. | 03.05 - 03.20 | Utambulisho (Wakurugenzi, Uongozi Na Watoa Huduma Kwa Mfuko) | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5. | 03.20 - 03.30 | Kupitia Muhtasari Kutoka Kwenye Mkutano wa Nne | Wote |
| 6. | 03.30 - 03.45 | Kupitia taarifa ya Yatokanayo Kutoka Kwenye Mkutano wa Nne | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7. | 03.45 - 04.00 | Taarifa ya Mwenyekiti | Mwenyekiti wa Bodi |
| 8. | 04.00 - 04.30 | Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka<br>1. Mwangalizi wa Mfuko<br>2. Mkaguzi wa Hesabu<br>3. Taarifa ya Hesabu | <br>CRDB<br>KPMG<br>Mkurugenzi Fedha na Mipango |
| 9. | 04.30 - 05.00 | Kupokea Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji | Mkurugenzi wa Uwekezajii |
| 10. | 05.00 - 05.35 | Kipindi cha Maswali na Majibu | Bodi/Watendaji |
| 11. | 05.35 - 05.45 | Kufunga Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |

# 2 Muhtasari wa Mkutano wa Nne (4) wa Mwaka

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA NNE (4) WA MWAKA WA MFUKO WA UKWASI ULIOFANYIKA JUMAMOSI YA TAREHE 19 NOVEMBA 2022 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM

## WALIOHUDHURIA (Kiambatisho "A")

### BODI YA WAKURUGENZI

1. Bw. Casmir S. Kyuki - Mwenyekiti wa Bodi
2. Dkt. Judika L. King'ori - Mjumbe wa Bodi
3. Bw. David E. Mwankenja - Mjumbe wa Bodi
4. Bw. Paul A. Maganga - Mjumbe wa Bodi
5. Bi. Neema J. Jones - Mjumbe wa Bodi
6. Bw. Simon M. Migangala - Mkurugenzi Mtendaji

### WAJUMBE WA KAMATI ZA BODI YA WAKURUGENZI

1. Bw. Lameck Kakulu - Mjumbe wa Kamati ya Bodi
2. Dkt. Fortunatus Magambo - Mjumbe wa Kamati ya Bodi

### WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1. Bw. Daniel Ole Sumayan - Mjumbe wa Kamati ya Bodi

### WAALIKWA

1. Bw. Vicent. Onjara - KPMG/Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko
2. Bi. Rashida Rashid - KPMG/Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko
3. Bw. Anandumi Meena - CRDB / Waangalizi wa Mfuko
4. Bi. Mariam Mtunguja - CMSA / Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana
5. Bi. Veronica Sanga - Mwakilishi wa Msajili wa Hazina

### MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS

1. Bw. S. Migangala
2. Bw. I. Wahichinenda
3. Bi. J. Msofe
4. Bi. P. Nchimbi
5. Bw. D. Mbaga
6. Bw. S. Bujiku
7. Bw. R. Mwanga
8. Bw. M. Kimario
9. Bi. J. Swai
10. Bw. P. Ndunguru
11. Bi. V. Abuogo
12. Bw. F. Bwalya
13. Bw. B. John
14. Bi. J. Mlimbila
15. Bw. D. Balima
16. Bw. M. Balati
17. Bw. H. Mnongane
18. Bw. B. Liwali
19. Bw. C. Chanjarika
20. Bw. J. Joseph
21. Bi. R. Maruma
22. Bw. J. Masoud
23. Bw. L. Chokola
24. Bw. B. Lukinga
25. Bw. A. Mushi
26. Bw. L. Temela
27. Bw. W. Ramadhan
28. Bi. J. Njovu
29. Bi. V. Maheri
30. Bi. D. Milenge
31. Bi. W. Malya
32. Bi. H. Lashkoni
33. Bw. A. Mabruk
34. Bw. A. Ambari
35. Bw. J. Nyambo
36. Bw. S. Ivambi
37. Bi. S. Kapufi
38. Bi. Y. Masanyoni
39. Bi. A. Laurent
40. Bi. E. Simon
41. Bw. M. Mchanjila
42. Bw. J. Mwangomola
43. Bi. M. Minja
44. Bi. M. Mashiku
45. Bw. F. Lushinge
46. Bi. D. David
47. Bw. S. Khatib
48. Bi. P. Kasilati
49. Bw. F. Mzoo
50. Bw. N. Muhoji
51. Bi. V. Mashindano
52. Bi. A. Omari
53. Bw. A. Kandila
54. Bi. L. Malimiru
55. Bi. A. Alex
56. Bw. D. Makassy
57. Bw. S. Rugaitika
58. Bi. T. Mpiluka
59. Bi. S. Mgaya
60. Bi. V. Yuda

### WENYE VIPANDE NA TAARIFA YA AKIDI

Wajumbe wenye Vipande waliohudhuria walikuwa 963 na majina yao yameambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi kama Kiambatisho "A". Mkurugenzi Mtendaji alitoa taarifa kwamba idadi ya Vipande vilivyowakilishwa ni 276,666,589.766 kati ya jumla ya Vipande 1,463,049,631.521 vya Mfuko. Kwa mujibu wa mahudhurio Vipande vilivyowakilishwa vilikuwa ni asilimia 18.9103 ya jumla ya Vipande vyote vya Mfuko na hivyo Mkutano ungeweza kuanza kwa sababu akidi inayohitajika kwenye Waraka wa Makubaliano (Deed of Trust) ni asilimia 10.

## DONDOO ZA MKUTANO

1. Utambulisho
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
3. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita
4. Taarifa ya Mwenyekiti
5. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko
6. Taarifa ya Wakaguzi wa Mfuko
7. Taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizokaguliwa
8. Taarifa ya Meneja wa Mfuko Kuhusu Uwekezaji
9. Kipindi cha Maswali na Majibu
10. Kufunga Mkutano

## UFUNGUZI WA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano saa tatu na robo asubuhi (03:15) kwa kuwakaribisha wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS, Wawekezaji na Wageni waalikwa waliohudhuria Mkutano.

## 1.0 UTAMBULISHO NA MAELEZO YA AWALI

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS aliwatambulisha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Mwakilishi wa Msajili wa Hazina, na Menejimenti ya Kampuni ya UTTAMIS. Vilevile aliwatambulisha wawakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko, Kampuni ya KPMG ambayo inatoa Huduma za Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko, pamoja na Wageni wengine waalikwa.

## 2.0 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Baada ya kuzipitia Kumbukumbu za Mkutano uliopita kifungu kwa kifungu, wajumbe wote kwa kauli moja walipitisha na kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano mkuu wa tatu (3) wa mwaka wa mfuko wa ukwasi pamoja na kumbukumbu za mkutano maalum wa mfuko wa ukwasi za tarehe 04 disemba 2021.

## 3.0 YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Hakukuwa na yatokanayo na Mkutano wa tatu (3) wa Mfuko wa Ukwasi. Hoja zote zilizotolewa zilijibiwa kwa ufasaha na hakukuwa na jambo la kufanyiwa kazi.

## 4.0 TAARIFA YA MWENYEKITI

4.1 Mwenyekiti aliwasilisha taarifa ya Mfuko wa Ukwasi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022. Taarifa ilieleza kama ifuatavyo: -

4.2 Mwenyekiti alianza kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye Mkutano Mkuu wa nne (4) wa Mwaka wa Wawekezaji wa Mfuko wa Ukwasi. Alitoa shukrani kwa wawekezaji wa Mfuko kwa kuendelea kuwa na imani na UTT AMIS hasa katika kipindi cha mwaka 2022 na kuendelea kufuatilia maendeleo ya Mfuko.

4.3 Taarifa ilieleza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, muhula wa utendaji wa wajumbe wanne wa Bodi ya Wakurugenzi ambao ni Bw. Juma Muhimbi, Dkt. Suleiman Mohamed, Bw. Ramadhani Hamisi na Bw. Francis Chachah ulifikia tamati tarehe 14 Aprili 2022. Shukurani zilitolewa kwa wajumbe hao kwa kumaliza muhula wao vizuri na kwa kazi nzuri ya kuijenga UTT AMIS katika kipindi chote walichohudumu. Wawekezaji walitaarifiwa pia kuwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alifanya uteuzi wa Wajumbe wapya wanne wa Bodi ya Wakurugenzi ya UTT AMIS. Shukurani zilitolewa kwa Mheshimiwa Waziri kufanya uteuzi huo lakini pia pongezi zilitolewa kwa wajumbe wapya walioteuliwa.

4.4 Mwenyekiti pia alieleza kwamba katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, utendaji wa Mfuko ulikuwa mzuri licha ya changamoto zilizojitokeza. Faida katika Mfuko imekuwa juu ya kigezo linganishi (Performance Benchmark) ikiwa ni wastani wa faida ya asilimia kumi na nne nukta mbili (14.2) ikilinganishwa na asilimia 9.3 ya kigezo linganishi. Alieleza kwamba katika kipindi chote hicho, thamani ya Mfuko iliendelea kukua pamoja na idadi ya wawekezaji kuongezeka kutokana na imani na uelewa kuhusu faida ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Pia ilielezwa kuwa thamani ya mfuko imeongezeka kutoka bilioni 215.9 kwa mwaka 2021 mpaka bilioni 434.7 kwa mwaka 2022.

4.5 Mwenyekiti alizidi kueleza kuwa, pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili Dunia ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine, viashiria vya kiuchumi vinaonyesha kwamba uchumi wa Tanzania umeendelea kufanya vizuri. Kwa mujibu wa machapisho ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Pato la Taifa (Gross Domestic Product) lilikua kwa asilimia 5.4 katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia tarehe 31 Machi 2022 na asilimia 4.8 kwa robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2022, ikilinganishwa na asilimia 4.9 na aslimia 4.3 za robo ya tatu na ya nne za mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ya robo mwaka iliyoishia

tarehe 30 Juni 2022, Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.4 katika nchi za Africa Mashariki na wastani wa asilimia 10.1 kwa nchi za ukanda wa SADC ukiondoa nchi ya Zimbabwe. Aidha, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita, viwango vya riba katika soko vilishuka, hatua ambayo ililenga kuongeza ukwasi kwenye sekta binafsi na kukuza shughuli za kiuchumi nchini. Kadhalika, thamani ya Shilingi ya Tanzania iliendelea kubaki imara dhidi ya Dola ya Marekani ambapo ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, kiwango cha kubadilisha Dola moja ya Marekani kiliongezeka kwa asilimia 0.2 wakati kwa Shilingi ya Uganda viwango vilishuka kwa asilimia 5.3 na kwa Shilingi ya Kenya viwango vilishuka kwa asilimia 8.3.

4.6 Kuhusu maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, ilielezwa kuwa utendaji hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi (Tanzania Share Index). Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022, Fahirisi imeonyesha kuwa na ongezeko la asilimia 7.5 kutoka 3653.0 tarehe 30 Juni 2021 hadi 3928.5 tarehe 30 Juni 2022 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.8 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021. Hali hii inamaanisha kwamba, katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2022, bei za hisa zilipanda zaidi ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Kati ya sababu zilizosababisha kupanda kwa bei za hisa ni pamoja na utendaji mzuri wa kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na uboreshwaji wa mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Shukurani zilitolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuweka sera na mazingira bora ya kufanya biashara na pia kwa kuweza kudhibiti athari zitokanazo na janga la UVIKO-19 na kuyumba kwa mfumo wa shughuli za kibiashara ulimwenguni.

4.7 Taarifa ilizidi kueleza kwamba, viashiria vya kiuchumi vinaonesha kuwa Kampuni ya UTT AMIS pamoja na mifuko inayoisimamia inaendelea kufanya vizuri. Thamani ya mifuko imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 612.8 tarehe 30 Juni 2021 hadi kufikia Shilingi bilioni 996.5 tarehe 30 Juni 2022. Ongezeko hili la kiasi cha Shilingi bilioni 383.7 ni sawa na asilimia 62.6 ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi bilioni 206.8 sawa na asilimia 50.0 kwa mwaka uliotangulia. Ilielezwa kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa UTT AMIS na mifuko yake kushuhudia ongezeko kubwa kama hili ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. Ongezeko la ukubwa wa mifuko limeenda sambamba na ongezeko la idadi ya wawekezaji 29,832 sawa na asilimia 17.0 waliojiunga katika mifuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 ikilinganishwa na wawekezaji 12,798 sawa na asilimia 8.0 waliojiunga katika mwaka wa fedha uliotangulia.

4.8 Pia ilielezwa kwamba Kampuni ya UTT AMIS inaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano utakaoishia mwezi Juni mwaka 2024. Katika Mpango Mkakati huo Kampuni imeazimia kujikita kwenye matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma kwa wawekezaji. Aidha, Miaka mitatu iliyopita Kampuni ya UTT AMIS ilizindua utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwa kutumia simu za kiganjani na inaendelea na uunganishwaji wa mifumo ya kibenki na mifumo ya UTT AMIS. Lengo la uunganishaji huu ni kuongeza ufanisi kwa kupunguza mlolongo wa hatua za uchakataji wa miamala inayofanywa kwa njia za kibenki. Kufuatia kukamilika kwa uunganishaji wa mifumo ya UTT AMIS na mifumo ya Benki ya CRDB, ambao pia ni Waangalizi wa mifuko, Kampuni ya UTT AMIS imesaini makubaliano ya uunganishaji wa mifumo na benki za NMB, NBC, Exim, Stanbic na ABSA na kwamba miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hii inategemewa kuongeza idadi ya miamala itakapokamilika.

4.9 Taarifa ilieleza kwamba idadi ya miamala inayofanywa kwa njia ya simu imeongezeka kufikia wastani wa Shilingi bilioni moja na nusu kwa mwezi kutoka wastani wa Shilingi milioni mia saba kwa mwezi katika mwaka wa fedha uliopita. UTT AMIS inaendelea vizuri ingawa bado haijafika kwenye kilele cha matumizi ya kufanya miamala ya uwekezaji kwa njia hii ya kidijitali. Hivyo Kampuni ya UTT AMIS itaendelea kutoa elimu ya manufaa ya matumizi ya njia za kidijitali katika uwekezaji huku ikiendelea kuwekeza katika mifumo mipya ya huduma kwa wawekezaji pamoja na kuimarisha usalama katika mifumo hiyo.

4.10 Mwisho, Mwenyekiti alihitimisha taarifa yake na kuwashukuru wawekezaji wote kwa ushirikiano na imani yao kwenye Kampuni ya UTT AMIS na Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Aidha,

kwa namna ya kipekee Mwenyekiti aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wenzake wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa UTT AMIS na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha UTT AMIS kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Mwenyekiti alimalizia kwa kusema ana matumaini makubwa kuwa ushirikiano huo utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini.

## 5.0 TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO

5.1 Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko wa Ukwasi, aliwasilisha Taarifa iliyoeleza kwamba jukumu lao ni kusimamia na kuhakikisha kwamba utendaji wa Meneja wa Mfuko unazingatia Waraka wa Makubaliano ili kuhakikisha masilahi bora ya wenye Vipande.

5.2 Mwakilishi huyo alieleza kuwa katika utekelezaji wa kazi yao kama Mwangalizi wa Mfuko, wana majukumu mbalimbali yakiwemo uangalizi wa mali za Mfuko, kuhakikisha Meneja wa Mfuko anatumia njia au mbinu sahihi kukokotoa mahesabu ya thamani ya Mfuko sambamba na Waraka wa Makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa na kusaidiana na Meneja wa Mfuko katika kukusanya fedha, kuwafikia wateja pamoja na kuwasaidia kuuza vipande vyao.

5.3 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichoishia tarehe 30 Juni 2022, benki ya CRDB, kama Mwangalizi wa Mfuko wa Ukwasi, wameendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za Meneja wa Mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

5.4 Mwakilishi wa Benki ya CRDB alihitimisha kwa kuwathibitishia Wawekezaji wa Mfuko kwamba shughuli za uwekezaji kwenye Mfuko wa Ukwasi na wajibu wa Meneja wa Mfuko vimeendeshwa na kutekelezwa kufuatana na vipengele vya Waraka wa Makubaliano na kwamba maslahi ya wenye Vipande ndani ya Mfuko wa Ukwasi yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo.

## 6.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MFUKO WA UKWASI

6.1 6.1 Mwakilishi kutoka Shirika la Wahasibu la KPMG ambao ni Wakaguzi wa Mfuko aliwasilisha Muhtasari wa Taarifa kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022. Alieleza kuwa Muhtasari wa Taarifa ya Hesabu za Mfuko zilizowasilishwa yaani Taarifa ya Mapato na Matumizi, Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

6.2 Taarifa ilieleza kuwa Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha hauoneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (International Financial Reporting Standards (IFRS). Taarifa ya wakaguzi iliendelea kusema kwamba Muhtasari huu wa hesabu za kifedha pamoja na hii taarifa yao siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Pia ilielezwa kwamba Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

6.3 Pia taarifa ilieleza kwamba maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 27 Oktoba 2022 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Taarifa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022 inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wahesabu za Mfuko.

6.4 Mwakilishi huyo alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa majukumu yao kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zao za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards on Auditing–ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), kuhusu “Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za fedha”.

## 7.0 TAARIFA YA MWAKA KUHUSU HESABU ZA MFUKO WA UKWASI

7.1 Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Hesabu za Mfuko kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

7.2 Mkurugenzi aliwaomba wawekezaji kusoma taarifa kwa kulinganisha hali ya utendaji wa Mfuko kwa miaka miwili (2) iliyoishia mwezi Juni 2022 na 2021.

7.3 Ilielezwa kuwa Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu nne, ambazo ni Taarifa ya Mapato na Matumizi (Statement of Profit or Loss and Other Comprehensive Income), Taarifa ya Urari wa Hesabu za Mfuko (Statement of Financial Position), Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko (Statement of Changes in Net Assets Attributable to Unit Holders) na Taarifa ya Mtiririko wa Fedha (Statement of Cash Flows).

7.4 Kwa upande wa Mapato na Matumizi, Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, jumla ya Mapato ya Mfuko yalikuwa Shilingi 51,786,000,000/= ikilinganishwa na Mapato ya Shilingi 26,668,408,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Ongezeko hili linatokana na weledi wa meneja wa Mfuko katika kusimamia uwekezaji. Pia ilielezwa kuwa jumla ya Gharama za Uendeshaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 ilikuwa Shilingi 8,903,487,000/= ikilinganishwa na Shilingi 3,875,338,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021, hivyo kufanya Mapato baada ya kutoa gharama za uendeshaji na kabla ya kodi kuwa Shilingi 42,882,513,000/= ikilinganishwa na Mapato ya Shilingi 22,793,070,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Kodi iliyotozwa na Serikali ilikuwa Shilingi 324,896,000/= ikilinganishwa na Shilingi 56,652,000/= kwa mwaka wa fedha 2021. Hivyo, Mfuko ulibaki na Faida Halisi (baada ya Kodi na Matumizi) ya Shilingi 42,557,617,000/= ikilinganishwa na Shilingi 22,736,418,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

7.5 Kwa upande wa Urari wa Hesabu za Mfuko, ilielezwa kuwa Rasilimali za Mfuko zilikuwa ni Shilingi 438,824,543,000/= mnamo tarehe 30 Juni 2022 ikilinganishwa na Shilingi 226,315,802,000/= tarehe 30 Juni 2021. Dhima za Mfuko zilikuwa na jumla ya Shilingi 2,320,107,000/= mnamo tarehe 30 Juni 2022, ikilinganishwa na Shilingi 4,094,080,000/= tarehe 30 Juni, 2021. Kutokana na Taarifa hiyo, Thamani halisi ya Mfuko tarehe 30 Juni, 2022, ilikuwa ni Shilingi 436,504,436,000/= ikilinganishwa na Shilingi 222,221,722,000/= tarehe 30 Juni 2021.

7.6 Katika Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko ilielezwa kuwa, Thamani ya Mfuko Mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2022 ilikuwa Shillingi 222,221,722,000/= ikilinganishwa na Shillingi 111,289,045,000/= Mwanzoni mwa Mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2021. Ongezeko kutokana na faida ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2022 ilikuwa ni Shilingi 42,557,617,000/= ikilinganishwa na Shilingi 22,736,418,000/= kwa mwaka linganishi ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Kwa upande wa Miamala ya wenye vipande Mfuko ulifanya mauzo ya vipande vya Shilingi 543,031,923,000 ukilinganisha na mauzo ya vipande vya mwaka 2021 yalikuwa ni Shilingi 285,562,973,000 wakati ununuzi wa Vipande ulikuwa Shilingi 371,306,826,000 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021 mauzo yalikuwa ni Shilingi 197,366,714,000.Hii ilipelekea ongezeko zaidi (net sales) kiasi cha Shillingi 171,725,097,000/= Kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2022 ikilinganishwa na Shilingi 88,196,259,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Kutokana na Mwenendo huo imepelekea mabadiliko ya thamani halisi ya Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, kuwa Shilingi 436,504,436,000/= ikilinganishwa na Shilingi 222,221,722,000/= kwa mwaka 2021.

7.7 Kwa upande wa Taarifa ya Mtiririko wa Fedha, ilielezwa kuwa fedha halisi iliyotokana na shughuli za uendeshaji kabla ya marekebisho ya mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022, ilikuwa Shilingi 42,557,617,000/= ikilinganishwa na Shilingi 22,736,418,000/= kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Aidha fedha halisi iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za Uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji na kodi ya Serikali ilikuwa Shilingi 192,890,317,000/= ikilinganishwa na Shilingi 70,917,564,000/= kwa mwaka wa fedha 2021. Miamala kwa wawekezaji ilipelekea ongezeko (net sales) la shilingi 171,725,097,000/= tarehe 30 Juni 2022 ikilinganishwa na shilingi 88,196,259,000/= tarehe 30 Juni 2021. Matumizi hayo yalipelekea punguzo halisi la fedha kiasi cha Shillingi 21,165,220,000/= Mwaka wa fedha uliosha 30 Juni 2022 ikilinganishwa na

ongezeko la Shillingi 17,278,695,000/= Tarehe 30 Juni 2021. Aidha Mfuko ulikuwa na akiba ya Fedha kiasi cha Shilingi 22,108,999,000/= Mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022 ikilinganishwa na Akiba ya fedha kiasi cha Shilingi 4,830,304,000/= Mwanzoni mwa Mwaka wa Fedha 2021, Hivyo kupelekea Mfuko kubaki na Akiba ya fedha kiasi cha Shilingi 943,779,000/=, mwishoni mwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 ikilinganishwa na Akiba ya fedha kiasi cha Shilingi 22,108,999,000/=, mwishoni mwa mwaka linganishi wa 2021.

## 8.0 TAARIFA YA MENEJA WA MFUKO KUHUSU UWEKEZAJI

8.1 Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya UTT AMIS aliwasilisha Taarifa ya Meneja kuhusu uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

8.2 Taarifa ilieleza kuwa, Mfuko wa Ukwasi uliendelea kupata mafanikio makubwa katika Ukuaji wa thamani ya kipande na ukubwa wa Mfuko. Thamani halisi ya kipande iliongezeka kutoka shilingi 281.9 hadi kufikia shilingi 321.9, sawa na faida ya asilimia 14.2 kwa mwaka. Ukubwa wa mfuko uliongezeka kwa shilingi billioni 218.8 kutoka shilingi bilioni 215.9 mnamo Juni, 2021 hadi shilingi bilioni 434.7 mnamo 30 Juni, 2022.

8.3 Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22, UTTAMIS kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi alionao katika kuhakikisha mfuko unafikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwenye uwekezaji wake wenye kuleta tija huku akizingatia sera na miongozo mbalimbali inayotumiwa kwenye uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 mgawanyo anuai wa rasilimali za mfuko ilikuwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali namba II. Mfuko wa Ukwasi umewekeza kiasi cha asilimia 89.9 kwenye dhamana za serikali za muda mrefu, asilimia 10.0 kwenye amana za benki za muda maalumu na asilimia 0.1 kwenye amana za benki za muda mfupi.

8.4 Faida ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia Juni 2022 ilikuwa asilimia 14.2 ikilinganishwa na faida ya asilimia 15.3 kwa mwaka 2021. Mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Ukwasi na maeneo linganifu yalielezwa.

8.5 Kuhusu pato la Taifa, meneja alisema kuwa Kwa mwaka 2021 uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 4.9, ukilinganisha na kiwango cha asilimia 4.8 mwaka 2020. Hata hivyo kutokana na kuwepo kwa wimbi na athari mbaya za UVIKO-19 (COVID-19). Pato la taifa mwaka 2020 lilishuka kwa asilimia 2.2. Kwa kipindi cha mwaka 2022, uchumi unakadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 5.2 kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazoendelea nchini. Mtazamo wa ukuaji ni muhimu kwa mipango iliyosimamiwa na UTT AMIS na uchumi kwa ujumla kwani husaidia kudumisha na kuimarisha thamani ya uwekezaji nchini. Hali imara na stahimilivu juu ya mwenendo wa uchumi nchini ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na UTT AMIS na maeneo mengine ya uwekezaji nchini. Hata hivyo uchumi imara husaidia kutunza na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi.

8.6 Hali ya mfumuko wa bei nchini kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022 ni asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 3.6 iliyonakiliwa Juni 2021. Kwa kipindi hicho, mfumuko wa bei uliongezeka huku sababu kuu zikitajwa kuwa ni ongezeko la bei ya mafuta, vifaa vya ujenzi na vyakula (mahindi, ngano, viazi vitamu, mihogo na mchele). Hali ya uchumi nchini na mwenendo wa mfumuko wa bei ni stahimilivu kiasi ambacho kimewezesha wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji kuwekeza kwa wingi. UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida shindani kuliko kiwango cha mfumuko wa bei.

8.7 Kuhusu Sekta ya benki, Meneja alieleza kuwa Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni 2022 hali ya utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa imara kwani jumla ya rasilimali na amana ziliongezeka. Ongezeko kwenye rasilimali ni shilingi trilioni 6.0 (asilimia 15.1) kutoka shilingi trilioni 39.7 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 45.7 mwaka 2022. Jumla ya amana kwenye benki iliongezeka kwa shilingi trilioni 2.7 (asilimia 10.0) hadi kufikia shilingi trilioni 29.6 kutoka shilingi trilioni 26.9. Jumla ya mikopo imefikia shilingi trilioni 25.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na shilingi trilioni 21.4 mwaka uliopita. Ubora wa rasilimali ambao unapimwa kwa uwiano wa mikopo isiyolipika na rasilimali kwa ujumla umeimarika kutoka asilimia 9.3 mwezi Juni 2021 hadi asilimia 8.2 mwezi Aprili 2022. Kuendelea kuimarika

kwa sekta ya benki ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kwa ujumla kwani huduma zitolewazo na benki huchochea ufanisi kwenye uchumi.

8.8 Kuhusu Dhamana za Serikali ilielezwa kuwa Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni 2022, Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ilipunguza kiasi cha dhamana za serikali za muda mfupi sokoni ikilinganishwa na mwaka uliopita. Kiasi hicho cha dhamana kilipunguzwa kwa takribani shilingi trilioni 0.3 (asilimia 13.6) kutoka shilingi trilioni 2.2 hadi shilingi trilioni 1.9. Hata hivyo, Uhitaji wa dhamana za serikali za muda mfupi uliongezeka kwa asilimia 26.0 (shilingi trilioni 0.6) hadi kufikia shilingi trilioni 2.9 kutoka shilingi trilioni 2.3 mwaka wa 2021. Aidha, kiasi kilichochukuliwa baada ya mnada kimeongezeka kwa asilimia 6.6 (shilingi trilioni 0.1) kutoka shilingi trilioni 1.5 hadi shilingi trilioni 1.6 Juni 2022. Kwa kipindi hicho, kiasi cha dhamana za serikali za muda mrefu kilichouzwa kwenye soko la awali ni shilingi trilioni 3.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.0 mwaka uliopita.

8.9 Kiwango cha ushiriki kwenye minada hiyo kiliongezeka hadi shilingi trilioni 6.4 (asilimia 33.3) ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.8. Aidha kiwango kilichokubaliwa na Benki Kuu ya Tanzania baada ya mnada kilipunguzwa kwa shilingi trilioni 0.3 (asilimia 10.0) hadi shilingi trilioni 2.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.0 mwaka 2021. Kwa kipindi cha mwaka mmoja hali ya ushiriki wa wawekezaji kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ilikuwa kubwa ikilinganishwa na ushiriki kwenye dhamana za muda mfupi. Ongezeko hilo la ushiriki liliongezeka kutoka asilimia 7.8, mwezi Julai 2021 hadi asilimia 14.6 mwezi Mei 2022 huku sababu kuu ikiwa ni kuongezeka kwa elimu ya uwekezaji hususani katika eneo hilo.

8.10 Kuhusu viwango vya Riba katika dhamana za serikali za muda mfupi zilipungua kutoka wastani wa asilima 3.6 mwezi Juni 2021 hadi asilimia 3.0 mwezi Juni 2022. Viwango vya riba jumuishi za mikopo katika benki za biashara ni asilimia 16.2 ikilinganishwa na asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021. Uwekezaji kwenye amana za benki kwa muda wa mwaka mmoja zilitoa faida ya asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka 2021. Viwango vya hifadhi ya akiba kisheria vya Benki kuu kwa benki za biashara pamoja na punguzo la riba nchini viliendelea kuwa asilimia 7.0 na 5.0. Mabadiliko ya riba katika soko la fedha na mitaji huathiri moja kwa moja thamani ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kiujumla. Vivyo hivyo kuongezeka kwa riba sokoni hupelekea kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji kwenye mifuko hususani pindi uwekezaji mpya unapofanyika.

8.11 Kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia mwezi Juni 2022, viwango vya kubadilisha fedha kati ya Shilingi ya kitanzania na fedha za kigeni vimeendelea kuwa stahimilivu. Thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya Marekani ilikuwa imara na ya kuridhisha, ingawa ilipungua kidogo kwa asilimia 0.2 kutoka Shilingi 2,310.4 Juni 2021 hadi Shilingi 2,315.7 Juni 2022. Uimara wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na serikali kwa ujumla kwani inasaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo thamani yake ipo katika shilingi za kitanzania na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania.

8.12 Kuhusu Soko la Mitaji na dhamana, taarifa ilieleza kuwa kwa muda wa mwaka mmoja ulioisha mwezi Juni 2022 kumekuwa na viashiria chanya katika miamala na shughuli kwenye soko la mitaji na dhamana. Mwezi Februari 2022 soko lilianzisha Hatifungani ya benki ya NMB toleo la nne (4) yenye ukomo wa miaka mitatu (3) na faida ya asilimia 8.5. Hatifungani hiyo ilifanikiwa kupata ushiriki mkubwa mara mbili zaidi ya kiwango cha fedha kilichotarajiwa.

Kwa upande wa dhamana za serikali za muda mrefu, kuanzia mwezi Novemba 2021 Benki kuu ilianzisha utaratibu wa kutoa uwekezaji kwa mara ya pili (re-issue) kupitia soko la awali. Vilevile, mwezi Aprili 2022 Benki kuu ilipunguza viwango vya riba/faida kwenye dhamana hizo. Hivyo basi, kuanzishwa na kuwepo kwa ongezeko la ushiriki na miamala sokoni kunatoa viashiria na matarajio chanya kwa wawekezaji wa ndani, nje ya nchi na uchumi kwa ujumla.

8.13 Taarifa ya Soko la Upili kwa dhamana na Hatifungani zilizoorodheshwa ilionyesha kuwa Kiwango cha ushiriki kwenye eneo la dhamana za serikali na hatifungani za kampuni binafsi kimeongezeka ingawa viwango vya faida vimepungua ikilinganishwa na mwaka uliopita. Mauzo ya dhamana za serikali za muda mrefu yaliongezeka kwa shilingi trilioni 1.0 (asilimia 45.4) kutoka shilingi trilioni 2.2 mwaka uliopita

(Juni 2021) hadi shilingi trilioni 3.2. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2022, thamani jumuishi ya mauzo kwa upande wa Hatifungani za kampuni binafsi zilipungua hadi shilingi bilioni 0.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.7 Juni 2021. Hadi Juni 2022 kulikuwa na jumla ya kampuni mbili (2) zilizoorodheshwa zenye hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 104.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 120.0 iliyonakiliwa Juni 2021. Aidha, Kiwango cha thamani kwa hatifungani za kampuni binafsi kilipungua kwa asilimia 12.6 kutokana na kuiva kwa hatifungani ya benki ya NMB (T3) na EXIM. Hatifungani zilizopo ni za benki ya NMB (T4), na Taasisi ya Mikopo ya nyumba kwa benki nchini (TMRC T1, T2 & T3).

8.14 Kuhusu Soko la Hisa taarifa ilionyesha kuwa hali ya mauzo ya Hisa na shughuli sokoni ilipungua kwa takribani shilingi bilioni 405.3 (asilima 76.1) kutoka shilingi bilioni 531.9 hadi shilingi bilioni 126.6 tarehe 30 Juni 2022. Vilevile, Ukubwa wa mtaji wa soko ulipungua thamani kwa shilingi trilioni 0.9 (asilimia 5.4) hadi shilingi trilioni 15.6 kutoka shilingi trilioni 16.5.

Katika kipindi cha mwaka mmoja kampuni zifuatazo zilitangaza na kulipa gawio; TCC (Tsh. 800.0), TPCC (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 255), benki ya NMB (Tsh. 193.4), DSE (Tsh. 100.6), na benki ya CRDB (Tsh. 36) kwa kila hisa. Hivyo basi, kwa wawekezaji wote waliowekeza kwenye kampuni tajwa walipata gawio sawa na maelezo hapo juu.

8.15 Taarifa ilionyesha kuwa hadi tarehe 30 Juni 2022 jumla ya rasilimali kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS imefika shilingi bilioni 996.5 kutoka shilingi bilioni 612.8. Rasilimali ziliongezeka kwa asilimia 62.6 sawa na shilingi bilioni 383.7 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 197.5 iliyonakiliwa mwaka uliopita. Kwa kipindi chote hadi Juni 2022 kumekuwa na muamko wa uwekezaji kwenye mifuko, hali iliyopelekea ongezeko kubwa la rasilimali. Meneja aliwahakikishia wawekezaji wake kuwa itaendelea kubuni na kuvumbua mianya na fursa za uwekezaji kadri inavyojitokeza katika soko ili kuongeza mapato na faida kwa wawekezaji. Lengo likiwa ni kuvuka matarajio ya wawekezaji kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## 9.0 MASWALI, MAONI NA MAJIBU

### 9.1 Wenye vipande waliuliza maswali pamoja na kutoa hoja zifuatazo:-

9.1.1 Pongezi nyingi zilitolewa kwa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa UTT AMIS kwa kusimamia mifuko vizuri na weledi wa hali ya juu na kuhakikisha faida inapatikana vizuri.

9.1.2 Mwekezaji aliomba ufafanuzi kutoka kwenye taarifa ya mwaka ya mfuko, hususani sehemu ya dondoo za kikao kilichopita mwaka 2021 kwani taarifa hiyo haikuwa imesainiwa na mwenyekiti.

9.1.3 Kuhusu taarifa za kikao kilichopita, mwekezaji aliuliza ni hatua gani imefikiwa kwenye utekelezaji wa pendekezo lililotolewa mwaka jana (2021) la kuwepo kwa dawati la huduma za UTT kwenye matawi ya benki ya CRDB nchini kote kwa lengo la kusogeza zaidi huduma kwa jamii.

9.1.4 Mwekezaji aliuliza ni kwa nini taarifa ya hesabu ya mfuko inayopatikana kwenye taarifa ya mwaka haitoi taarifa zote? Vilevile, mwekezaji aliendelea kwa kuuliza sababu iliopelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka 2021.

9.1.5 Ufafanuzi ulihitajika kuhusu mikakati aliyonayo meneja wa mifuko ili aendelee kutoa faida nzuri sokoni kwani hali ya soko kupitia viashilia vyake vinaonesha faida kwenye sehemu nyingi za uwekezaji nchini inapungua mwaka hadi mwaka. Mwekezaji aliendelea kutoa mfano kwa kurejea taarifa ya mwaka ya mfuko ukurasa namba 36 jinsi mfumuko wa bei nchini unavyozidi kuongezeka pamoja na kupungua kwa viwango vya faida nchini.

9.1.6 Mwekezaji aliuliza ni kwa nini utaratibu wa malipo kwa mwekezaji alieuza vipande kwenye mfuko wa Ukwasi unachukua siku nyingi zaidi ya tatu (3) zilizoainishwa kwenye waraka wa makubaliano (offer document)?

9.1.7 Mapendekezo yalitolewa na wawekezaji juu ya kuwa na mpango wa kutoa mkono wa pole endapo mwekezaji akifariki, au utaratibu ukoje endapo mwekezaji atafariki.

9.1.8 Mwekezaji aliomba ufafanuzi kutoka kwa mwakilishi wa benki ya CRDB juu ya kutokuwepo kwa utaratibu wa kutumwa

pesa kwenda UTT kwa mpango wa kila mwezi (standing order.

9.1.9 Wawekezaji waliishauri bodi ya UTT iangalie njia mbadala ya mwekezaji kuuza vipande kwa njia ya simu.

9.1.10 Ufafanuzi ulihitajika juu ya tofauti iliyopo kati ya mapato na rasilimali.

9.1.11 Mwekezaji alishauri elimu ya uwekezaji hususani kwenye mifuko ya UTT itolewe kwa wingi.

9.1.12 Ufafanuzi ulihitajika juu ya muundo wa UTT na je wafanyakazi hulipwa na serikali au UTT.

9.1.13 Mwekezaji alianza kwa kupongeza hali ya utendaji na kisha aliuliza, UTT inajipanga vipi na Watumishi housing, Taasisi ambayo imeanzisha mfuko wa uwekezaji wa pamoja (Faida Fund)

9.1.14 Mwekezaji aliomba maelezo juu ya utekelezaji wa vitambulisho kwa wawekezaji.

9.1.15 Mwekezaji aliomba maelezo ya kina juu ya mipango iliyopo ili kuepukana na wizi wa fedha kibenki na mitandao kiujumla.

9.1.16 Mwekezaji alitaka ufafanuzi juu ya utaratibu uliopo, endapo mwekezaji akitaka kuchukua mkopo kwenye taasisi za benki kwa dhamana ya uwekezaji wake kwenye mifuko.

9.1.17 Wawekezaji walitoa ushauri na mapendekezo juu ya namna nyingine nzuri ya kuongeza rasilimali au ukubwa wa mfuko kama hali ya ongezeko ilivyo nzuri mwaka 2022. Walishauri idadi ya wawekezaji ichapishwe kwenye makablasha ya mwaka, meneja afanye juhudi ili kuwafikia watanzania waishio nje ya nchi (diaspora), Meneja kuitumia na kushirikiana na benki ya NMB na nyinginezo na UTT AMIS itumie watu maarufu na vikundi kwenye jamii ili kuwafikia watu wengi zaidi.

9.1.18 Maelezo yalihitajika juu ya faida ya asilimia 14.2 iliyopatikana mwaka 2022, faida hii ni ya muda gani na huwekwa wakati gani kwenye uwekezaji wa kila mwekezaji. Mwekezaji aliendelea kuuliza juu ya kigezo cha ufanisi je ni nini maana yake, na kinapatikana kwa kutumia njia gani?

9.1.19 Mwekezaji alishauri UTT iangalie maeneo mengine ya uwekezaji kama vile kwenye sekta ya nishati na mawasiliano?

9.1.20 Ufafanuzi ulihitajika juu ya utaratibu uliopo wa kuhamisha uwekezaji kutoka mfuko wa Ukwasi kwenda mifuko mingine. Mwekezaji aliuliza ni kwa nini namba za bure za mawasiliano (toll free) za UTT hazipokelewi?

### 9.2 Wawakilishi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS walitoa ufafanuzi na kujibu maswali kama ifuatavyo:-

9.2.1 Pongezi zilipokelewa na Meneja wa mfuko na kuahidi kuendelea kusimamia kwa weledi na maarifa ili kuwaletea faida zaidi katika uwekezaji wao.

9.2.2 Kuhusu kutokuwepo kwa saini ya Mwenyekiti kwenye dondoo za mkutano uliopita mwaka 2021. Ufafanuzi ulitolewa na mwakilishi wa UTT AMIS akasema, utaratibu wa kusaini taarifa hiyo ni baada ya kuletwa kwenye kikao cha mwaka ili wawekezaji wazipitie, waziidhinishe na kisha Mwenyekiti kusaini.

9.2.3 Kuhusiana na utoaji wa elimu na kuwepo kwa huduma za UTT AMIS kwenye matawi yote ya benki ya CRDB nchini. Mwakilishi kutoka benki ya CRDB alieleza ushirikiano uliopo kati ya benki na UTT AMIS kwani wameshaanza kutoa elimu kwa wafanyakazi wa benki nchini kote kwa njia ya mtandao (video conference) na hivyo huduma zinapatikana kwenye matawi yote ya CRDB nchini kote.

9.2.4 Kuhusu suala la kutokuwepo kwa taarifa yote kwenye taarifa ya mwaka ya mfuko hususani kwenye taarifa ya hesabu sambamba na swala la ongezeka la gharama za uendeshaji. Mwakilishi alisema taarifa hiyo imeandaliwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya utoaji taarifa za kifedha (Internation Financial Reporting Standards (IFRS)). Hata hivyo, mwakilishi aliwashauri wawekezaji watembelee tuvuti ya UTT ili wapate makablasha yenye taarifa zenye mchanganuo na rejea kwa kina (Notes to the Financial Statements).

9.2.5 Kuhusu kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, alieleza sababu ni kuongezeka kwa rasilimali au ukubwa wa mfuko kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka 2021 jambo hilo lilipelekea kuongezeka kwa gharama. Aidha, Kiwango cha kutoza gharama kisheria kinategemea ukubwa wa mfuko. Aliendelea kwa kuwahakikishia wawekezaji kuwa gharama hizo zimezingatia viwango vilivyopo kwenye waraka wa wakubaliano (Trust Deed).kwa kuzingatia faida kwa wawekezaji

9.2.6 Kuhusu mikakati dhidi ya mfumuko wa bei na kupungua kwa viwango vya faida kwenye

soko la mitaji na dhamana. Mwakilishi alisema UTT AMIS daima hujitahidi kuwekeza na kutoa faida ambayo ni kubwa kuliko kiwango cha mfumuko wa bei. Mwakilishi aliwatoa wasiwasi wawekezaji kuwa hali ya mfumuko wa bei nchini Tanzania ni stahimilivu na nzuri ikilinganishwa na mataifa mengine fanani hivyo basi wawekezaji waendelee kuiamini UTT AMIS. Mwakilishi alirejea takwimu za faida kwa mwaka 2022 ni asailimia 14.2 ikilinganishwa na mfumuko wa bei wa asilimia 4.4. Kuhusu kushuka kwa viwango vya faida alisema, utaratibu wa mabadiliko ya viwango vya faida sokoni hugunduliwa na husababishwa na mvutano wa faida na uwepo wa fursa za uwekezaji ikilinganishwa na mahitaji na msukumo wa uwekezaji (demand and supply). Hivyo basi, kilichosababisha kushuka kwa viwango hivyo ni nguvu za soko na sio Benki kuu kama wengi wanavyosema. Mabadiliko hayo katika soko ni hali ya kawaida na ni afya katika shughuli za uwekezaji sokoni.

9.2.7 Kuhusu ufafanuzi wa ucheleweshwaji wa malipo pindi wawekezaji wanapotoa pesa au kuuza vipande. Mwakilishi aliomba radhi kwa wawekezaji waliopatwa na adha hio, kisha akasema utaratibu ni ule ule hufanyika ndani ya siku tatu (3) za kazi tangu UTT AMIS itakapopokea maombi hayo ofisini au kupitia barua pepe. Mwakilishi aliendelea kusema UTT AMIS ipo kwenye matazamio ya kuendelea kuboresha huduma hii na alikiri kupokea mapendekezo mbalimbali likiwemo la kutuma na kutoa uwekezaji kwa kutumia simu ya mkononi (mobile wallet) yote hayo yamepokelewa na UTT AMIS inaahidi kuyafanyia kazi.

9.2.8 Kuhusu mrithi endapo mwekezaji amefariki. Mwakilishi kutoka UTT AMIS alieleza kuwa wakati wa ufunguzi wa akaunti ya uwekezaji, mwekezaji anatakiwa kuweka jina au majina ya warithi ili ikitokea amefariki mrithi aendelee au atumie uwekezaji huo. Endapo mwekezaji hakumtaja mrithi au warithi basi UTT AMIS itafuata maelekezo ya mahakama.

9.2.9 Ufafanuzi ulitolewa na mwakilishi kutoka benki ya CRDB kuhusu huduma ya utoaji wa pesa mfululizo kwa mpango wa kila mwezi kwa ridhaa ya mteja (standing order). Mwakilishi alisema kwa sasa wawekezaji wanaweza kuomba huduma hiyo na aliwashauri kutumia huduma ya benki kwa mtandao (internet banking) huduma ambayo wataifanya wao wenyewe bila kufika tawini kwa kutumia simu janja au vifaa vingine.

9.2.10 Ufafanuzi ulitolewa kwa wawekezaji kuhusu ushauri uliotolewa wa kuuza na kupata malipo ya vipande (repurchase) kwa njia ya mitandao ya simu za mkononi. Mwakilishi alisema, kwa sasa UTT AMIS inaendelea na utaratibu wake wa kulipa maombi ya kuuza vipande kwa njia ya benki. Aidha, mwakilishi aliwashukuru wawekezaji kwa michango na ushauri wao na aliahidi kupokea ushauri huo na UTT AMIS itaendelea kulitazama swala hilo kwa kuzingatia usalama wa fedha na thamani.

9.2.11 Kuhusu ufafanuzi wa mapato na rasilimali, mwakilishi alitoa maelezo kuwa mapato ni fedha iliyozalishwa kwenye mfuko kutokana na shughuli za uwekezaji au shughuli nyinginezo wakati Rasilimali ni jumla ya fedha au mali zote katika mfuko.

9.2.12 Suala la utoaji wa elimu ya mfuko kwa watanzania, ufafanuzi ulitolewa kuwa Meneja wa mfuko anafanya jitihada kubwa kuhakikisha elimu ya mifuko ya UTT AMIS inawafikia watanzania wengi ili waweze kunufaika na mifuko. Mpaka sasa meneja amekuwa akifanya matangazo ya mifuko na faida zake kupitia redio mbalimbali, kuhudhulia semina na vikao vya wadau mbalimbali, Magazeti vilevile kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya Habari. Hii yote ni kuhakikisha UTT AMIS inawafikia watanzania kwa ujumla wao waweze kunufaika na Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

9.2.13 Kuhusu muundo wa UTT AMIS na ulipaji mishahara kwa wafanyakazi, mwakilishi alitoa ufafanuzi kuwa UTT AMIS ni Taasisi ya serikali iliyopo chini ya wizara ya fedha na mipango. Fedha za uendeshaji wa Taasisi hii hupatikana kwa utaratibu wa kutoza gharama za uendeshaji (management fee) kwenye mifuko na huduma sambamba na viwango vilivyopo kwenye waraka wa makubaliano (Trust Deed). Aidha, kupitia utaratibu huo UTT AMIS (Meneja) hupata fedha zinazosaidia kuendesha na kulipa wafanyakazi pamoja na matumizi mengine. Mwakilishi aliendelea kusisitiza kuwa gharama zote zinazotozwa kwenye mifuko zipo kisheria kama ilivyoainishwa kwenye waraka na ikitokea kuna gharama zaidi ya uwezo wa mfuko basi kiasi hicho hulipwa na meneja (UTT AMIS).

9.2.14 Kuhusu suala la vitambulisho au kadi za kieletroniki kwa wawekezaji, ufafanuzi ulitolewa kuwa UTT AMIS imeanza mchakato

wa kuboresha utambulisho na taarifa kwa wawekezaji wake na kwa sasa zoezi la kutoa vitambulisho lipo tayari. Aidha, mwakilishi aliwakaribisha wawekezaji kujaza fomu za maombi ya kitambulisho kwa mwekezaji atakaehitaji.

9.2.15 Kuhusu suala la kuwepo kwa mfuko uitwao Faida (Faida fund) ulioanzishwa na Taasisi ya Watumishi housing, mwakilishi alisema sekta ya uwekezaji hususani kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kwa ujumla, Taasisi au kampuni za usimamizi wa mifuko (fund managers) wanatakiwa wawe wengi ili iwe chachu na afya kwa uchumi. Aidha, aliongeza kwa kusema meneja wa mifuko wakiwa wengi husaidia kuleta hali ya ukwasi, faida na ushindani sokoni. Mwakilishi alimalizia kwa kusema Taasisi ya Watumishi housing ni Taasisi ya serikali kama UTT AMIS ilivyo na wanashirikiana katika maeneo mbalimbali na hivyo, wawekezaji ndio watakao chagua yupi anafaa ikilinganishwa na mwingine.

9.2.16 Kuhusu wizi, mwakilishi alisema swala hilo HALIPO NA HALIJAWAHI KUTOKEA. Alisema, tangu mwaka 2005 hakujawahi kuwa na tatizo hilo kwa sababu ya kuwepo kwa mifumo mahiri ya kupokea na kulipa fedha za wawekezaji. Aidha, muundo huu kwenye mifuko unasaidia sana kutofautisha na kutenganisha majukumu kati ya UTT AMIS, benki (CRDB), mkaguzi (auditors) na wadau wengine hii hurahisisha na kuleta ufanisi katika utendaji.

9.2.17 Ufafanuzi ulitolewa juu ya namna faida na utoaji fedha kwenye uwekezaji. Mwakilishi alisema kiwango cha faida hutokana na shughuli za uwekezaji na hali ya soko na endapo mwekezaji akitoa fedha basi kiasi hicho hupunguza idadi ya vipande vyenye thamani sawa na fedha y. Mwakilishi alirejea jedwali namba moja (I) akasema kwa mwaka 2022 faida ni asilimia 14.2 hii inamaanisha kwa mwekezaji aliewekeza kwa kipindi tangu tarehe moja Julai 2021 hadi 30 Juni 2022 bila kutoa wala kuongeza amepata faida hiyo. Aidha, kwa uwekezaji wa shilingi milioni kumi (10.0) faida ya asilimia 14.2 ni sawa na ongezeko kwenye mtaji la kiasi cha shilingi milioni moja na laki nne na ishirini elfu (1,420,000). Kiasi hiki cha faida kinawekwa na ni jumuishi (cumulative) kwenye mtaji kwa kila siku kulingana na utendaji wa soko kwa siku husika. Endapo mwekezaji atataka kiasi chochote cha pesa siku yoyote tangu awekeze ni ruksa kuchukua, alete maombi ya kutoa fedha na UTT AMIS itamlipa ndani ya siku tatu za kazi. Kuhusu kigezo cha ufanisi, alitoa maelezo kuwa hiki ni kiwango cha faida sokoni ambacho mfuko wa ukwasi hulinganishwa nacho. Aidha, alisema kiwango cha kigezo linganishi ni faida kwenye dhamana ya serikali ya miaka saba (7) ambapo kwa mwezi wa sita (6) tarehe 30 mwaka 2022 kiwango hicho ni asilimia 9.3 ikilinganishwa na asilimia 14.2 ya mfuko wa Ukwasi.

9.2.18 Kuhusu kutopokelewa simu kwa namba za bure za huduma kwa wawekezaji. Mwakilishi aliwaomba radhi wawekezaji waliokumbwa na adha hiyo na alisema watalifanyia kazi ili kuboresha zaidi.

9.2.19 Kuhusu diaspora, yaani watanzania waishio nje ya nchi. Mwakilishi alieleza kwa sasa wawekezaji hao wanashiriki uwekezaji kwenye mifuko kwa njia ya barua pepe hususani kwenye kukamilisha usajili wao na pindi wanapotaka huduma ya kuuza vipande (repurchase). Aidha, benki ya CRDB ambae ni mwangalizi wa mifuko pamoja na benki zingine zina huduma ya kibenki inayowawezesha kuwekeza pesa moja kwa moja (system intergration) kwenye uwekezaji wao kwa kutumia mtandao (internet banking). Aidha, elimu kwa wawekezaji hao hutolewa kwa njia ya mtandao, mikutano kwa video (video conference) pamoja na simu za mkononi (whatsap call)

## 10. KUFUNGA MKUTANO

Kwa kuwa hakukuwa na masuala zaidi ya kujadili, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS aliwashukuru Wawekezaji wote kwa kuhudhuria katika Mkutano huo. Pia aliwahakikishia ya kuwa mawazo na mapendekezo yaliyotolewa katika Mkutano yatazingatiwa na yale yanayowezekana yatatekelezwa. Mwisho aliwatakia heri ya sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya 2024. Mkutano ulifungwa saa 6:09 mchana.

.................................. ..................................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

..................................

**TAREHE**

## KIAMBATISHO "A"

### ORODHA YA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA UKWASI WALIOHUDHURIA KWENYE MKUTANO MKUU ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 19 NOVEMBA 2022

| S/NO | JINA LA MWEKEZAJI |
|---|---|
| 1 | ABDILLAH HASSAN MOHAMED |
| 2 | ABEID MUSTAFA MAWAKA |
| 3 | ABIGAIL ANGELUS MAKUA |
| 4 | ABISSAY HUSSEIN NDAKI |
| 5 | ABRAHAMU MAGODA NZOWA |
| 6 | ABUBAKARI MUSSA KIBUNYUNYA |
| 7 | ADA AHMEDI MAPONMDELA |
| 8 | ADAM IDDY URASSA |
| 9 | Adela Elibariki Lyimo |
| 10 | ADELAIDA NDESOLO RIMISHO |
| 11 | ADELINA ALPHONCE KANINKA |
| 12 | ADVENTINA MARY LWAKATARE |
| 13 | AEA CROWDFUNDING |
| 14 | AGAPE AMADEUS KAMAGENGE |
| 15 | AGNES HENRY MAKULE . . |
| 16 | AGNES LAWRANCE CHIBWANA |
| 17 | AGNES NGOLLE NYONI GODDA |
| 18 | AGNES PONERA KONDOWE . . |
| 19 | AIDAN ADRIANO |
| 20 | AIDELY STEPHAN CHAWALA |
| 21 | AISHA HASSAN WAZIRI |
| 22 | AISHER MOHAMED KIRAVU |
| 23 | AIZECK ANDREW KALAGO |
| 24 | ALBERT ANACLET IKONJE |
| 25 | ALBERT BENSON KIMARO |
| 26 | ALBERT ERNEST SWAI |
| 27 | ALBINA BENEDICT MINDE BURRA |
| 28 | ALEX ALEXANDER MASENENE |
| 29 | ALEX JEREMIAS KOBALYENDA |
| | **505,876,088** | **264,779,339** |
| **Miamala (Transactions) ya wenye vipande kwa mwaka** | | |
| Mauzo ya vipande (Sales) | 771,604,107 | 543,031,923 |
| Ununuzi ya vipande (Repurchase) | (555,635,410) | (371,306,826) |
| **Mabadiliko ya thamani ya mfuko** | **215,968,697** | **171,725,097** |
| **Thamani halisi ya Mfuko** | **721,844,785** | **436,504,436** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO (CASH FLOW STATEMENT) KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2023

| | 2023<br>TSH '000 | 2022<br>TSH '000 |
|---|---|---|
| **FEDHA ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | |
| Ongezeko la Thamani (Mapato) baada ya Kodi | 69,371,652 | 42,557,617 |
| **Imerekebishwa na:** | | |
| Gharama ya Kodi | 329,428 | 324,896 |
| Faida/(Hasara) itokanayo na mauzo ya Dhamana za Serikali | (71,493,690) | (41,114,849) |
| Faida/(Hasara) itokanayo na uwekezaji kwenye taasisi za fedha | (2,131,205) | (3,248,951) |
| **Faida kabla ya mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji:** | **(3,923,815)** | **(1,481,287)** |
| **Mabadiliko ya Mtaji wa uendeshaji** | | |
| Amana za muda maalum katika taasisi za kifedha | 38,000,000 | (42,912,857) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhamana za serikali | (325,388,405) | (183,067,086) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhima | 7,442,242 | (1,773,973) |
| Ongezeko /(Kupungua) kwa Dhima ambazo hazijapokelewa | (120,565) | (23,288) |
| **Fedha iliyotumika kwenye shughuli za uendeshaji** | **(283,990,543)** | **(229,258,491)** |
| Kodi ya Zuio iliyolipwa | (329,428) | (324,896) |
| Mapato yaliyopokelewa kwenye uwekezaji wa dhamana za serikali | 63,979,512 | 35,541,772 |
| Mapato yaliyopokelewa kwenye uwekezaji wa taasisi za kifedha | 3,949,336 | 1,151,298 |
| **Fedha halisi iliyotumika kwa shughuli za uendeshaji** | **(216,391,123)** | **(192,890,317)** |
| **AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES)** | | |
| Mauzo ya Vipande (Sales of Units) | 771,604,107 | 543,031,923 |
| Ununuzi wa Vipande (Repurchase) | (555,635,410) | (371,306,826) |
| **Fedha halisi iliyotokana na miamala ya wenye vipande** | **215,968,697** | **171,725,097** |
| **Ongezeko/(Punguzo) halisi la Fedha** | **(422,426)** | **(21,165,220)** |
| **Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka** | **943,779** | **22,108,999** |
| **Salio la fedha mwishoni mwa Mwaka** | **521,353** | **943,779** |

....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** Novemba, 2023

....................................
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** Novemba, 2023

# 8 Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji

# Taarifa ya Meneja kuhusu Uwekezaji

Mfuko wa ukwasi ulianzishwa mwezi Aprili 2013. Ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja ambao hutoa fursa kwa Taasisi na watu binafsi kuwekeza kipato chao cha ziada kwa kipindi kifupi cha kati au muda mrefu kwa faida na ukwasi madhubuti.

Mahitaji ya awali ya uwekezaji ni shilingi laki moja (100,000/=) na kiwango cha nyongeza sio chini ya shilingi elfu kumi (10,000). Mwekezaji anaruhusiwa kuchukua fedha zake wakati wowote anapohitaji na hulipwa ndani ya siku tatu (3) za kazi bila kutozwa gharama za kutolea [exit load], hivyo kudhihirisha kuwa mfuko wa ukwasi ni fursa maridhawa kwa wawekezaji.

## 1.0 Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande

Ukubwa wa Mfuko uliongezeka kwa shilingi bilioni 290.0 sawa na ongezeko la asilimia 66.7 kutoka shilingi bilioni 434.7 mnamo Juni, 2022 hadi shilingi bilioni 724.7 mnamo Juni, 2023. Katika kipindi hicho, thamani ya kipande iliongezeka kwa shilingi 40.2 kutoka shilingi 321.9 hadi shilingi 362.1, sawa na faida ya asilimia 12.5 kwa mwaka.

*Chati Na. I: Ukubwa na thamani ya kipande kwa mfuko wa Ukwasi hadi tarehe 30 Juni 2023.*




## 2.0 Mgawanyo wa Uwekezaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 mwezi Juni 2023, UTT AMIS kama meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali kwa matakwa ya sera za mfuko wa Ukwasi. Mgawanyo anuai wa rasilimali za mfuko mwezi Juni 2023 ulikuwa kama inavyoonekana kwenye chati namba II hapo chini:

*Chati Na. II: Mgawanyo wa Uwekezaji wa mfuko wa Ukwasi hadi tarehe 30 Juni 2023*

Chati namba II inaonesha mgawanyo wa uwekezaji katika mfuko wa ukwasi. Mfuko umewekeza zaidi kwenye dhamana za serikali za muda mrefu kwa kiasi cha asilimia 99.2, asilimia 0.7 kwenye amana za benki za muda maalumu na asilimia 0.1 iliwekezwa kwenye amana za benki za muda mfupi. Aidha, uwekezaji katika amana za benki za muda mfupi (call account) umefanywa ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa mfuko ikiwemo kulipa fedha kwa wawekezaji pindi wanapouza vipande vyao.




KUANZAISHWA;

APRILI, 2013

THAMANI YA KIPANDE SHILINGI 100.0

30 JUNI 2023

THAMANI YA KIPANDE

SHILINGI 362.1

UKUBWA WA MFUKO SHILINGI BILLION 724.7

FAIDA KWA MWAKA

12.5%

## 3.0 Faida

Faida ya mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 12.5 ikilinganishwa na faida ya asilimia 14.2 iliyonakiliwa mwaka uliopita (2022). Aidha, faida ya asilimia 12.5 ni tafsiri ya ongezeko la thamani kwenye mtaji wa mwekezaji aliewekeza kwa muda wa mwaka mmoja.

Kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba I hapo chini faida ilipungua kutoka asilimia 14.2 Juni 2022 hadi asilimia 12.5 juni 2023. Aidha, sababu kuu ya kupungua kwa kiwango cha faida ni kutokana na kupungua kwa viwango vya faida sokoni kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba V ikihusisha mtawanyo wa uwekezaji kwenye chati namba II.

***Jedwali Na. I: Faida ya mfuko wa Ukwasi tangu Juni, 2019 hadi Juni, 2023***

| Na | Mwaka wa Fedha | Ukubwa wa mfuko Shilingi Bilioni | Hali ya Utendaji | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Faida | Kigezo cha ufanisi |
| 01 | 2022/23 | 724.7 | 12.5% | 9.7% |
| 02 | 2021/22 | 434.7 | 14.2% | 9.3% |
| 03 | 2020/21 | 215.9 | 15.3% | 10.1% |
| 04 | 2019/20 | 112.8 | 15.1% | 2.3% |
| 05 | 2018/19 | 46.9 | 11.4% | 3.7% |

*Kumb: Faida kwenye Dhamana ya serikali ya miaka 7.*

Jedwali namba I hapo juu linaonesha mwenendo wa utendaji wa mfuko pamoja na kigezo cha ufanisi (benchmark). Hali ya utendaji wa mfuko inaonekana ni nzuri na shindani ikilinganishwa na kigezo cha ufanisi na maeneo linganifu, ambapo kwa mwaka 2023 faida ni asilimia 12.5 ikilinganishwa na asilimia 9.7.

Ili kupima mafanikio ya mfuko inabidi kulinganisha faida ya mfuko wa ukwasi na viwango linganifu vya faida vinavyotolewa na soko kwenye amana za benki na dhamana za serikali kama zilivyoainishwa kwenye jedwali namba II hapo chini

***Jedwali Na. II: Viwango vya faida katika Dhamana za Serikali na Amana za benki***

| Riba/Muda | Kwa Mwaka Wa Fedha Ulioisha Mwezi Juni | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 10 | 12.5% | 11.5% | 10.3% | 11.1% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 7 | 11.4% | 10.0% | 9.3% | 9.7% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 5 | 11.2% | 9.1% | 8.9% | 9.7% |
| Dhamana ya Serikali ya Miaka 2 | 8.1% | 7.6% | 4.4% | 9.1% |
| Dhamana ya Serikali ya Mwaka 1 | 4.6% | 4.8% | 3.9% | 6.9% |
| Amana za benki | 2.3% | 1.9% | 1.4% | 1.6% |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

Mambo mengine muhimu ya kuzingatia wakati wa kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Ukwasi na amana katika benki;

- Viwango vya riba vilivyoonyeshwa hapo juu ni kabla ya kutoa kodi ya zuio (withholding tax) ya asilimia 10.0 wakati mapato ya mfuko wa Ukwasi ni baada ya kutoa kodi ya zuio ya asilimia 10.0.
- Jambo lingine la muhimu la kuzingatia ni kwamba mfuko wa ukwasi unaruhusu wawekezaji wake kuuza vipande vyao wakati wowote hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji.

- Hakuna gharama wakati wa kuingia na kutoka katika mfuko.
- Aina nyingine ya uwekezaji katika masoko ya fedha zina muda maalum wa ukomo wake, uwekezaji katika mfuko wa ukwasi hauna muda maalum wala ukomo.

Kuwekeza kwenye mfuko wa ukwasi kuna faida zaidi ya kuwa na akaunti ya amana kwa sababu inamuongezea mwekezaji kipato kikubwa kutokana na viwango bora vya faida vinavyotolewa na mfuko.

## 4.0 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### 4.1 Pato la Taifa

Kwa mwaka 2022 uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 4.7, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.9 mwaka 2021 (kama ilivyooneshwa kwenye jedwali III). Hata hivyo, Kilimo, Ujenzi na Madini vilikuwa vichocheo vikubwa vya ukuaji wa uchumi katika kipindi hicho. Uchumi kwa mwaka 2023 unakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 5.2, ukichagizwa na kufufuliwa kwa shughuli za kiuchumi hususani uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi nchini.

Pato la taifa hutafasiri kiwango na shughuli za uchumi katika nchi. Hali imara na stahimilivu juu ya mwenendo wa uchumi nchini ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na UTT AMIS na maeneo mengine ya uwekezaji nchini. Uchumi imara husaidia kutunza na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

***Jedwali Na. III: Mwenendo wa ukuaji wa Uchumi Tanzania***

| Mwaka | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pato halisi la Taifa | 6.8% | 7.0% | 7.0% | 4.8% | 4.9% | 4.7% | *5.2% |

**Taarifa za makadirio, Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Benki kuu ya Tanzania (BOT)*

### 4.2 Mfumuko wa Bei

Hali ya mfumuko wa bei nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 ni asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 iliyonakiliwa tarehe 30 Juni 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini kunaashiria gharama za bidhaa na huduma mbalimbali zilipungua kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo Juni 2022.

Katika Jedwali IV hapo chini linaonyesha viwango vya mfumuko wa bei kwenye uchumi ulikuwa mzuri na kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka huu kimekuwa chini ikilinganishwa na mwaka uliopita.

***Jedwali Na. IV: Hali ya Mfumuko wa Bei***

| Mwaka | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa Bei | 3.4% | 3.7% | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.4% | 3.6% |

*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Hali ya uchumi nchini na mwenendo wa mfumuko wa bei ni stahimilivu kiasi ambacho kimewezesha wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji kuwekeza kwa wingi. UTT AMIS inajitahidi kuwekeza kwenye maeneo yanayotoa faida shindani kuliko kiwango cha mfumuko wa bei.

### 4.3 Sekta ya benki

Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia tarehe 30 Juni 2023, hali ya utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa stahimilivu na yenye faida. Mifumo ya malipo kwa njia ya kidigitali nchini iliendelea kuwa imara, ikithibitishwa na kuwepo kwa kiwango cha juu cha miamala iliokamilika kwa muda mfupi. Aidha, kuwepo kwa mifumo imara na thabiti kumehamasisha umma kuendelea kuamini na kutumia mifumo kwenye huduma mbalimbali za kifedha.

Jumla ya rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi trilioni 45.7 iliyonakiliwa Juni 2022 hadi shilingi trilioni 53.7 Juni 2023. Ongezeko kwenye rasilimali ni shilingi trilioni 8.0, sawa na asilimia 17.5. Kiasi cha amana kiliongezeka kwa shilingi trilioni 5.7 sawa na asilimia 20.3 kutoka shilingi trilioni 28.0 Juni 2022 hadi shilingi trilioni 33.7 Juni 2023.

Jumla ya mikopo imefikia shilingi trilioni 31.5, sawa na asilimia 21.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 25.9 mwaka uliopita. Ongezeko kwenye kiwango cha mikopo lilisababishwa na kupungua kwa masharti na viashiria vya hatari miongoni mwa wateja. Hata hivyo, viashiria vya hatari kwenye mikopo ya wateja wadogo na Taasisi zisizo za kifedha vilipungua ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na uchumi kwa ujumla kwani huduma zitolewazo na benki huchochea ufanisi kwenye uchumi. Aidha, hadi tarehe 30 Juni 2023 meneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja amefanikiwa kuunganisha mifumo ya UTT AMIS na benki ili kuwawezesha wawekezaji kununua vipande kidigitali, hivyo kurahisisha uwekezaji mahali popote.

## 4.4 Sekta ya Mawasiliano

Ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini umechagizwa na ongezeko la watu, huduma bora, na kuongezeka kwa matumizi ya simu janja. Idadi ya watumiaji wa huduma za simu imeongezeka kwa milioni 7.8 sawa na asilimia 13.8 kutoka milioni 56.2 mwaka jana hadi kufikia milioni 64.0 Juni mwaka huu. Usajili wa huduma za kifedha kupitia simu (idadi ya akaunti) umeongezeka kwa milioni 9.8, sawa na asilimia 26.2 kutoka milioni 37.4 hadi milioni 47.2 Juni 2023.

Sekta hii imeendelea kutawaliwa na kampuni kubwa zenye nyenzo nzuri za tehama, uvumbuzi na ubunifu hali ambayo imepelekea kujipatia idadi kubwa ya wateja na soko nchini.

Kwa kipindi chote, ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini umeleta matokeo chanya kwa Taasisi ya UTT AMIS kwani imechochea na kurahisisha uwekezaji katika mifuko na kuboresha zaidi huduma binafsi. Aidha, kupitia simu za mkononi wawekezaji wanaweza kufungua akaunti, kununua vipande na kuangalia salio na miamala waliofanya kwa kupiga ***150*82#** au kwa kutumia programu tumizi (UTT AMIS APP). UTT AMIS inatarajia kukamilisha na kuruhusu maombi ya uuzaji wa vipande yafanyike kupitia simu za mikononi ili kufanya huduma zote za Uwekezaji zifanyike kidigitali mahali popote walipo.

UTT-AMIS pia inaendelea kutumia majukwaa mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii kufikia umma kwa urahisi zaidi, katika mawasiliano na elimu juu ya uwekezaji. Mitandao hio ni pamoja na Facebook, Twitter, Instagram, Youtube, pamoja na Whatsapp.

## 4.5 Dhamana za Serikali

Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioisha tarehe 30 Juni 2023, Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliongeza kiasi cha dhamana za serikali za muda mfupi sokoni kwa shilingi trilioni 1.4 sawa na asilimia 73.6 hadi shilingi trilioni 3.3 Juni 2023. Hata hivyo, Uhitaji wa dhamana za serikali za muda mfupi uliongezeka kwa asilimia 24.1 (shilingi trilioni 0.7) hadi kufikia shilingi trilioni 3.6 kutoka shilingi trilioni 2.9 mwaka jana. Aidha, kiasi kilichokubaliwa baada ya mnada kimeongezeka kwa asilimia 56.2 (shilingi trilioni 0.9) kutoka shilingi trilioni 1.6 hadi shilingi trilioni 2.5 Juni 2023. Kwa kipindi hicho, kiasi cha dhamana za serikali za muda mrefu kilichouzwa kwenye soko la awali kilikuwa ni shilingi trilioni 4.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.3 mwaka uliopita. Kiwango cha ushiriki kwenye minada hiyo kilipungua hadi shilingi trilioni 4.6 (asilimia 28.1) ikilinganishwa na shilingi trilioni 6.4. Aidha kiwango kilichokubaliwa na Benki Kuu ya Tanzania baada ya mnada kiliongezeka kwa shilingi trilioni 1.2 (asilimia 44.4) hadi shilingi trilioni 3.9 kikilinganishwa na shilingi trilioni 2.7 mwaka 2022. Kwa kipindi cha mwaka mmoja hali ya ushiriki wa wawekezaji kwenye dhamana za serikali za muda mrefu ilipungua ikilinganishwa na ongezeko la ushiriki kwenye dhamana za muda mfupi.

Ongezeko la ushiriki katika eneo la dhamana za serikali kuna saidia kuleta na kuboresha hali ya ukwasi na faida sokoni.

## 4.6 Viwango vya Riba na Faida

Faida katika dhamana za serikali za muda mfupi zilipungua hadi wastani wa asilima 3.5 mwezi Juni 2023 kutoka asilimia 4.1 mwaka jana (Juni 2022). Viwango vya riba/faida katika mikopo (riba) na amana (faida) viliongezeka ikilinganishwa na viwango vilivyonakiriwa mwaka uliopita. Aidha, viwango vya riba jumuishi za mikopo katika benki za biashara ni asilimia 16.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka 2022. Uwekezaji kwenye amana za benki kwa muda wa mwaka mmoja zilitoa faida ya asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2022. Viwango vya hifadhi ya akiba kisheria vya Benki kuu kwa benki za biashara pamoja na punguzo la riba nchini viliendelea kuwa asilimia 7.0 na 5.0 mtawaliwa.

Viwango vya faida kwenye dhamana za serikali za muda mrefu havikubadilishwa tangu mabadiliko hayo yalivyofanyika mwezi wa nne (4) mwaka 2022.

*Jedwali Na. V: Mabadiliko kwenye viwango vya faida (coupon rate) kwenye Dhamana za Serikali za muda mrefu*

| Muda (Miaka) | 2 | 5 | 7 | 10 | 15 | 20 | 25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango kabla ya mabadiliko | 7.82% | 9.18% | 10.08% | 11.44% | 13.50% | 15.49% | 15.95% |
| Viwango baada ya mabadiliko | 7.60% | 8.60% | 9.48% | 10.25% | 11.15% | 12.10% | 12.56% |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

Kwa ujumla, kupungua kwa viwango vya faida kwenye maeneo ya uwekezaji huathiri faida ya wawekezaji kwenye mifuko inayosimamiwa na Taasisi ya UTT AMIS pamoja na maeneo linganifu.

## 4.7 Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Viwango vya kubadilisha fedha kati ya Shilingi ya kitanzania na fedha za kigeni vimeendelea kuwa stahimilivu nchini. Thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya kimarekani ilikuwa imara na ya kuridhisha ikisaidiwa na kuwepo kwa hali nzuri kwenye bei za bidhaa na huduma nchini. Kulingana na Jedwali hapa chini, linaonyesha kuwa thamani ya fedha nchini imebaki kuwa imara, ingawa, ilipungua thamani kidogo dhidi ya Dola ya Marekani kwa asilimia 1.0 (Tsh 23.4) hadi Tsh. 2,339.1 mwaka 2023 kutoka Tsh. 2,315.7 iliyorekodiwa mwaka uliopita.

*Jedwali Na. VI: Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni*

| Mwaka | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya Kubadilisha Fedha | 2,228.9 | 2,264.1 | 2,300.9 | 2,307.9 | 2,310.4 | 2,315.7 | 2,339.1 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

Ustahimilivu wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja ya UTT AMIS na Uchumi wa Tanzania kwa ujumla kwani husaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo thamani yake ipo katika shilingi za kitanzania. Kwa ujumla, Mifuko inayosimamiwa na UTT AMIS inatoa faida nzuri kwa Shilingi za Tanzania lakini inapobadilishwa hadi sarafu nyingine kama vile Shilingi ya Kenya au Dola ya Marekani faida inaweza kuathiriwa endapo kutakuwa na kupungua kwa thamani ya shilingi ya kitanzania katika kipindi hicho.

## 4.8 Soko la Mitaji na Dhamana

Kwa kipindi hadi juni 2023 soko la mitaji na dhamana limekuwa imara na thabiti, kwani limepelekea kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji katika soko la hisa, mitaji, dhamana na kwenye Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.

Soko limekuwa likifanya kazi vizuri kwa upande wa mauzo na shughuli mbalimbali, tuliona utoaji wa hatifungani mbili mpya za benki ya taifa ya biashara (NBC - Twiga) na benki ya biashara ya Kenya (KCB - Fursa Sukuk) zilizofanikiwa kufanya vizuri kwani jumla ya shilingi bilioni 49.9 zilipatikana. Mwezi Novemba 2022, Shirika la Watumishi Housing (WHI) lilizindua Mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaoitwa Faida (Mfuko wa Faida) ambao ulifanikiwa kuvutia wawekezaji na hadi disemba mfuko ulinakili shilingi bilioni 7.9. Ushiriki katika soko la mitaji na dhamana kwa wawekezaji wa ndani na nje umeimarika kutokana na umma kupata uelewa kuhusu uwekezaji na matumizi ya mifumo ya kidigitali.

Hali ya ushiriki kwenye soko la mitaji na dhamana nchini imeongezeka, ni matarajio yetu kuwa hali hii itazidi kuimarika na kuongezeka zaidi. Kuingia kwa Wasimamizi wapya wa Mifuko (Meneja wa Mifuko) ya uwekezaji wa pamoja na dhamana mpya sokoni ni ishara nzuri kwa UTT AMIS na soko kwa ujumla, na tunatarajia Taasisi au kampuni zingine kujiunga ili kuongeza ukwasi na ushindani sokoni jambo ambalo litaongeza zaidi ufanisi, faida na huduma bora.

### 4.8.1 Soko la Upili kwa Dhamana za serikali na Hatifungani za kampuni binafsi zilizoorodheshwa

Katika kipindi cha mwaka ulioishia juni 2023, kiwango cha ushiriki kwenye eneo la dhamana za serikali na kampuni binafsi kimeongezeka licha ya faida kuwa ya wastani.

Jumla ya dhamana za serikali kupitia soko la upili imeongezeka kwa shilingi trilioni 0.1, sawa na ongezeko la asilimia 3.1, hadi shilingi trilioni 3.3 kutoka shilingi trilioni 3.2 mwaka uliopita.

Jumla ya thamani za Hatifungani za kampuni binafsi iliongezeka kwa shilingi bilioni 0.1, sawa na asilimia 12.5 kutoka shilingi bilioni 0.8 Juni 2022 hadi shilingi bilioni 0.9 mwaka huu. Kupanda kwa Hatifungani hizo kulitokana na kuorodheshwa kwa hatifungani mpya za SUKUK na Twiga mwezi Desemba 2022.

Hatifungani za kampuni binafsi kwa sasa ni; Jasiri bondi ilioorodheshwa na benki ya NMB yenye ukomo wa miaka 3 na kiwango cha faida ya asilimia 8.5 kwa mwaka, Fursa Sukuk bondi ilioorodheshwa na benki ya KCB yenye ukomo wa miaka 3 na kiwango cha faida ya asilimia 8.75 kwa mwaka, Twiga bondi ilioorodheshwa na benki ya NBC yenye ukomo wa miaka 5 na kiwango cha faida ni asilimia 10 kwa mwaka na bondi ya miaka 5 ya Shirika linalotoa mikopo ya nyumba kwa benki nchini (TMRC) liliorodhesha kwa awamu kwa asilimia 10.48, 13.4607 na asilimia 11.79.

### 4.8.2 Soko la Hisa

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na kampuni 27 zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zenye mtaji wa jumla ya shilingi trilioni 15.0, ukubwa wa mtaji wa soko ulipungua thamani kwa shilingi trillioni 0.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.6 zilizorekodiwa mwaka uliopita.

Katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2023 shughuli za kibiashara katika soko la hisa zilishuka. Hii inadhihirishwa na kupungua kwa mauzo kutoka shilingi bilioni 126.6 hadi shilingi bilioni 107.6 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 19.0 sawa na asilimia 15.0. Fahirisi ya Hisa kwa kampuni za ndani za nchi (TSI) ziliongezeka kwa asilimia 4.1 hadi kufikia 4,091.8 huku Fahirisi ya Hisa zote (DSEI) ikipungua kwa asilimia 4.0 hadi 1,800.0.

Katika kipindi cha mwaka mmoja kampuni sita zilitangaza na kulipa gawio kwa wanahisa nazo ni; TCC/ Sigara (Tsh. 670.0), Twiga (Tsh. 390.0), TBL (Tsh. 290), benki ya NMB (Tsh. 286.0), SWISS (Tsh. 42.0), na benki ya CRDB (Tsh. 45) kwa kila hisa. Hivyo basi, kwa wawekezaji wote waliowekeza kwenye kampuni tajwa hapo juu walipata gawio sawa na maelezo hapo juu.

### 4.8.3 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Taasisi za usimamizi wa mifuko ya uwekekezaji wa pamoja nchini zinahusisha taasisi kuu mbili ambazo ni; Taasisi ya UTT Asset Management and investor Services (UTT AMIS), pamoja na shirika la watumishi housing (WHI) (Meneja wa mifuko). Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, Jumla ya rasilimali kwenye mifuko inayosimamiwa na Taasisi hizo ni shilingi bilioni 1,550.7.

#### 4.8.3.1 Mifuko ya Uwekezaji ya UTT AMIS

Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia Juni 2023, Mifuko ya uwekezaji inayosimamiwa na UTT AMIS kwa ujumla (Juni 2023) rasilimali ziliongezeka kwa shilingi bilioni 538.9 sawa na asilimia 54.0 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 383.7 sawa na asilimia 62.6 mwaka 2022. Katika kipindi hicho jumla ya rasilimali ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 996.5 tarehe 30 Juni 2022 hadi shilingi bilioni 1,535.4 tarehe 30 Juni 2023.

Ongezeko kwenye rasilimali za mifuko kunaashiria ongezeko kubwa la imani na uwekezaji kwenye mifuko inayosimamiwa na Taasisi ya UTT- AMIS. Aidha, ongezeko hilo limechangiwa na kiwango kwenye mauzo pamoja na faida kwenye maeneo ya uwekezaji.

#### 4.8.3.2 Shirika la Watumishi Housing (WHI) – Mfuko wa Faida

Shirika la Watumishi Housing (WHI) lilizindua Mfuko wa Faida mwezi Novemba 2022. Mfuko ulinakili rasilimali zenye thamani ya shilingi bilioni 7.9 Disemba 2022 na shilingi 100.3 kwa kila kipande. Kwa kipindi cha miezi sita tangu mauzo ya awali (IPO) hadi tarehe 30 Juni 2023 Mfuko ulikua kwa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 7.4 (asilimia 93.6) hadi shilingi bilioni 15.3 na thamani ya shilingi 104.9 kwa kipande.

***Vyanzo:*** *Benki kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, UTT AMIS, Watumishi Housing na Soko la hisa la Dar es Salaam.*

***Mwisho ninawatakia nyote msimu wa sikukuu uliojaa furaha tele na heri ya mwaka mpya wa 2024***

***Wekeza Uwezeshwe!***

# 9 Jarida la Habari

# Jarida la habari la UTT AMIS [Hadi tarehe 30 Septemba, 2023]

Uhuru kwa mwekezaj

| | |
|---|---|
| **1.0** | **Maelezo Mafupi juu ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS** |

- • Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023, kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS ina jumla ya mifuko ya uwekezaji wa pamoja sita (6) ijulikanayo kama; Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha,Mfuko wa Watoto, Mfuko wa jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani.
- UTT AMIS Inasimamia rasilimali zenye jumla ya thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.7.
- Mwaka 2017 Kampuni ya UTT AMIS ilianzisha huduma ya usimamizi wa mali kwa makampuni na watu binafsi inayoitwa UTT WEALTH MANAGEMENT yenye uwekezaji wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 26.9.
- Wawekezaji zaidi ya 264,610.
- Mifuko hutoa faida shindani katika soko.

| | |
|---|---|
| **2.0** | **Taarifa za ujumla za Mifuko iliyoanzishwa na kusimamiwa na kampuni ya UTT AMIS** |

| NA | JINA LA MFUKO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 2.1 | **Mfuko wa Umoja** | Mfuko huu ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2005.Mfuko wa wazi ambao hulenga wawekezaji wenye lengo la kuwekeza kwa muda mrefu. Sera ya mfuko huu ni kuwekeza kwenye soko la mitaji na dhamana. Baadhi ya sifa za mfuko huu ni kama zifuatavyo; |

- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi [hakuna gharama za kujiunga]
- Kiwango cha chini cha kujiunga ni vipande 10 tu
- Gharama ya kujiondoa inatozwa asilimia moja (1) ya thamani halisi ya kipande.
- Urahisi wa kujiunga na kutoka– manunuzi na mauzo hufanyika kila siku ya kazi
- Mauzo ya sehemu ya vipande yanaruhusiwa
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT-AMIS)

***Jedwali Na. 01; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023***

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tangu Kuanzishwa [Mei,2005]** | **10** | **7** | **5** | **2** | **1** |
| 15.5% | 27.4% | 14.3% | 13.5% | 13.2% | 13.1% |

***Chati Na. 01; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023***



**2.2** **Mfuko wa Wekeza Maisha**

Mfuko huu ulianzishwa tarehe 16 Mei, 2007. Mfuko unamwezesha mwekezaji kupata faida pacha, yaani mapato mazuri pamoja na mafao ya bima.

**Sifa za mfuko;**

- Taasisi na watu binafsi wenye umri kati ya miaka 18 na 55 ndio wanaoruhusiwa kujiunga
- Mfuko unatoa fursa za aina mbili za mpango wa kuchangia\kuwekeza: (a) Kuchangia kwa awamu na (b) Kuchangia kwa mkupuo mmoja.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [hakuna gharama za kujiunga]
- Kujiunga ni shilingi 8,340/- tu kwa mwezi [inatumika kama mpango wa kuchangia ni shilingi Milioni Moja]
- Mafao ya bima yanayopatikana ni:- Bima ya maisha, Bima ya ulemavu wa kudumu na Bima ya ajali.
- Mfuko unampa fursa mwekezaji kuwekeza kwa mpangilio maalum, mathalani anaweza kuchagua kuchangia kwa mwezi, mara mbili kwa mwaka au mara moja kwa mwaka

***Jedwali Na. 02; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023***

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kipindi cha Uwekezaji (Miaka) | | | | |
| **Tangu Kuanzishwa [Mei,2007]** | **10** | **7** | **5** | **2** | **1** |
| 14.0% | 31.7% | 23.5% | 25.5% | 15.0% | 14.2% |

***Chati Na. 02; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023***



# Watoto Fund
Faraja kwa Watoto

## 2.3 Mfuko wa Watoto

Mfuko wa Watoto unalengo la kuwawekea akiba Watoto kupitia uwekezaji kwa manufaa yao ya shule na maendeleo kiujumla Mfuko huu ulianzishwa tarehe 1 Oktoba 2008.

**Sifa za Mfuko;**

- Uwekezaji ni kwa ajili ya mtoto mwenye umri chini ya miaka 18.
- Kiwango cha chini cha uwekezaji kisichopungua shilingi 10,000/= na unaruhusiwa kuendelea kuwekeza kidogo kidogo kwa kiwango kisichopungua shilingi 5,000/=
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo. [ hakuna gharama za kujiunga ]
- Mfuko unatoa Mpango wa kukuza mtaji.
- Mwekezaji anaruhusiwa kuuzaa vipande vyake pindi mtoto anapofikisha umri wa miaka 12.

***Jedwali Na. 03; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023***

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kipindi cha Uwekezaji (Miaka) | | | | |
| **Tangu Kuanzishwa [Okt,2008]** | **10** | **7** | **5** | **2** | **1** |
| 12.9% | 25.1% | 16.4% | 16.8% | 14.1% | 13.3% |

***Chati Na. 03; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023***



Jikimu
Income Scheme
LIVE WELL ...YOU DESERVE IT

| 2.4 | **Mfuko wa Jikimu** | Mfuko huu ulianzishwa tarehe 3 Novemba 2008. Lengo la mfuko ni kukidhi mahitaji ya wawekezaji mfuko una wanaohitaji mapato ya mara kwa mara huku wakikuza mtaji kwa malengo ya muda wa kati na mrefu. |
|---|---|---|

**Sifa za Mfuko:**

- Mipango ya uwekezaji: (a) Mpango wa gawio wa robo mwaka [Kiwango cha chini cha uwekezaji ni Shilingi 2 Milioni], (b) Mpango wa gawio wa mwaka [Kiwango cha chini cha uwekezaji ni Shilingi 1 Milioni] na (c) Mpango wa mwaka wa kukua [Shilingi. 5,000/-]
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo [ hakuna gharama za kujiunga ]
- Gharama za kujitoa: Mfuko unatoza (a) asilimia 2.00 kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja (b) asilimia 1.5 kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya mwaka 1 na chini ya miaka 2(c) asilimia 1 kwa uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 2 na chini ya miaka 3 na (d) uwekezaji uliodumu ndani ya mfuko kwa kipindi cha zaidi ya miaka 3 hakuna gharama za kujitoa.
- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT-AMIS)

***Jedwali Na. 04; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023***

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kipindi cha Uwekezaji (Miaka) | | | | |
| **Tangu Kuanzishwa [Okt, 2008]** | **10** | **7** | **5** | **2** | **1** |
| 16.2% | 17.0% | 14.8% | 15.8% | 14.0% | 15.1% |

| Jumla ya Malipo ya Gawio [ID] tarehe 30 Septemba 2023 | | |
|---|---|---|
| **Taarifa** | **Shilingi Bilioni** | **Kwa kila kipande, shilingi** |
| Tangu Kuanzishwa [Oktoba,2008] | 16.0 | 173.5 |
| Mwaka Mmoja [Okt 22-Sept 23] | 1.0 | 12.0 |

***Chati Na. 04; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023***



FUND UKWASI
Uhuru kwa mwekezaj

2.5 **Mfuko Wa Ukwasi (Liquid Fund)**

Mfuko wa uwekezaji wa Pamoja ambao unatoa fursa ya uwekezaji mbadala kwa wawekezaji wanaopenda kuwekeza fedha zao za ziada kwa kipindi kifupi ama cha kati.

**Sifa za mfuko:**

- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha zake za mauzo ya vipande, (ndani ya siku 3 za kazi baada ya maombi ya kuuza vipande kupokelewa katika ofisi za UTT-AMIS makao makuu)
- Mfuko wa Ukwasi hautozi ada ya kujitoa wala kujiunga
- Mfuko unatoa unafuu wa gharama za uwekezaji
- Unafaa kwa wawekezaji Mmoja mmoja, vikundi na taasisi
- Kiwago cha chini cha uwekezaji ni shilingi 100,000 na uwekezaji wa nyongeza usiopungua ni shilingi 10,000.
- Mfuko unaruhusu uhamishaji wa vipande kutoka mwekezaji mmoja kwenda mwekezaji mwingine.
- Mfuko hauruhusu kuhamisha vipande kwenda kwenye mifuko mingine.
- Vipande vinauzwa kwa thamani halisi ya wakati huo[ hakuna gharama za kujiunga

***Jedwali Na. 05; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023***

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kipindi cha Uwekezaji (Miaka) | | | | |
| **Tangu Kuanzishwa [Apr, 2013]** | **10** | **7** | **5** | **2** | **1** |
| 26.0% | 25.2% | 21.0% | 18.1% | 13.6% | 12.3% |

***Chati Na. 05; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023***



2.6

## Mfuko wa Hati Fungani

## (Bond Fund)

Mfuko huu ulianzishwa tarehe 16 Septemba, 2019. Ni mfuko wa wazi ambao kiasi kikubwa kimewekezwa kwenye dhamana za serikali za muda mrefu. Mfuko una lengo la kutoa gawio, kulingana na faida itakayopatikana na kukuza mtaji kwa wawekezaji wenye lengo la muda wa kati na mrefu.

**Sifa za mfuko:**

Kuna aina tatu za mpango wa uwekezaji katika Mfuko huu:

- Mpango wa kukuza mtaji;
- Mpango wa gawio kila mwezi; na
- Mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

Kiwango cha chini cha kuanza kuweka.

(a) Shilingi 50,000 kwa mpango wa kukuza mtaji;

(b) Shilingi milioni 10 kwa mpango wa gawio kila mwezi; na

(c) Shilingi milioni 5 kwa mpango wa gawio kila baada ya miezi sita.

- Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT-AMIS)

*Jedwali Na. 06; Faida kwa kipindi hadi tarehe 30 Septemba 2023*

| Faida [%] Hadi Septemba 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| Tangu Kuanzishwa [Sept, 2019] | Kipindi cha Uwekezaji (Miaka) | | |
| | 3 | 2 | 1 |
| 14.9% | 14.8% | 13.4% | 12.2% |

| Jumla ya Malipo ya Gawio [ID] tarehe 30 Septemba 2023 | | |
|---|---|---|
| Taarifa | Shilingi Bilioni | Kwa kila kipande, shilingi |
| Tangu Kuanzishwa [Sept,2019] | 39.1 | 45.0 |
| Mwaka Mmoja [Okt 22 - Sept 23] | 21.0 | 12.0 |

*Chati Na. 06; Ukubwa wa Mfuko na Thamani ya Kipande tangu kuanzishwa hadi 30 Septemba 2023*



| | | |
|---|---|---|
| 2.7 | **Huduma ya usimamizi mali / UTT Wealth Management** | Huduma hii imejikita zaidi kumsikiliza mteja na kumtengenezea uwekezaji kulingana na mahitaji yake na uhalisia wa soko.<br><br>**Sifa**<br><br>Wawekezaji wote, binafsi, mashirika au Taasisi zilizopo ndani na nje ya nchi.<br><br>**Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza**<br><br>(a) Shilingi Millioni 100 kwa mpango wa kukuza mtaji, gawio au malipo;<br><br>**Gharama**<br><br>Asilimia 1 ya rasilimali kwa mwaka.<br><br>**Mkataba na Sera ya uwekezaji**<br><br>Uwekezaji huundwa na kusimamiwa kwa kufuata matakwa na mahitaji ya mwekezaji sambamba na lengo.<br><br>**Hali ya utendaji hadi tarehe 30 Septemba 2023**<br><br>• Ina jumla ya rasilimali zaidi ya shilingi bilioni 26.9;<br>• Faida kwa wawekezaji waliopo ni wastani zaidi ya asilimia 12.<br>• Ni rahisi kwa mwekezaji kupata fedha pindi anapohitaji, (ndani ya siku 3 za kazi baada ya kupokelewa katika ofisi za UTT-AMIS) |
| **3.0** | **Elimu kwa Wawekezaji** | |
| 3.1 | **Unawezaje kujiunga na Mifuko ya UTT AMIS?** | Mwekezaji anatakiwa kujaza na kukamilisha Fomu ya Maombi ya Kujiunga na Mfuko na kuweka fedha katika akaunti ya Mfuko kupitia matawi ya benki ya CRDB na madalali wote walioidhinishwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam.<br><br>Baada ya kukamilisha kufungua akaunti na taratibu zote za utambuzi (KYC), mwekezaji anaweza kuwekeza kwa kutumia simu ya mkononi kwa kupiga msimbo wa *150*82# au programu tumizi ya UTT AMIS ambayo inaweza kupakuliwa kutoka kwenye "App Store" au "Play store". Taratibu za kina zimetolewa kwenye fomu ya maombi.<br><br>• Tembelea ofisi za Kampuni ya Uwekezaji ya UTT (UTT AMIS) zilizopo Dar es Salaam na Dodoma, madalali wa soko la hisa la Dar es Salaam au tawi lolote la benki ya CRDB nchini. Pia piga simu za bure kwa namba zifuatazo: 0754800455 au 0754800544 [Kwa watumiaji wa voda] au 0715800455 au 0715800544 [kwa watumiaji wa tigo] na kwa watumiaji wa airtel 0782800455 ili uweze kupata 'Akaunti Namba' ya uwekezaji.<br>• Baada ya hapo, nenda tawi lolote la benki ya CRDB kuweka kiasi cha pesa unachopenda kuwekeza. [tafadhali hakikisha unaandika nambari yako ya uwekezaji katika fomu ya kuweka pesa ya CRDB]. Pia unaweza kutumia Kuwekeza kwa Kutumia mtandao wa simu wa Tigo Pesa, M-pesa na Airtel money. |

**3.2 Nini maana ya Mfumuko wa bei? Na jinsi gani inamuathiri mtu wa kawaida?**

Kwa tafsiri rahisi, mfumuko wa bei ni ongezeko la bei katika bidhaa na huduma katika uchumi kwa kipindi fulani. Wakati bei za bidhaa na huduma zinapopanda, matokeo yake ni kushuka kwa thamani ya fedha. Hivyo, uwezo wa fedha wa kununua bidhaa na huduma hupungua.

Kuna sababu nyingi za kiuchumi zinazopelekea kutokea kwa hali hii, hususani ongezeko la fedha katika mzunguko kusikoendana na kasi ya ukuaji wa Uchumi na hivyo matokeo yake kupelekea mfumuko wa bei.

Kiujumla, vigezo vilivyokubalika kupima viwango vya mfumuko wa bei ni pamoja na Bei za bidhaa za Jumla (Wholesale Price Index)], Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index), Mabadiliko ya pato la ndani la nchi (GDP) n.k . Vile vile, Bei za mahitaji ya kawaida ya walaji (Consumer Price Index) inapima gharama za bidhaa mbalimbali za msingi zinazotumiwa na kundi la watu ikiwakilisha makundi yote ya jamii kama kigezo cha upimaji wa uchumi katika nchi.

Ni muhimu kutambua kuwa, kazi ya kuangalia hali ya mfumuko wa bei katika nchi hufanywa na Benki Kuu. Kazi ya ufuatiliaji na kuchukua hatua stahiki katika kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei inachukua muda.

Jambo la msingi la kujifunzani kuwa, Katika uchumi wenye mfumuko wa bei, unashauriwa kuwekeza mara kwa mara hata kama kiasi cha kuwekeza ni kidogo. Kwa kujenga nidhamu ya uwekezaji, unaweza usione madhara au athari hasi za kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika uwekezaji.

**3.3 Nini maana ya Kompaundi?**

Kwa ufupi, ni faida inayopatikana kutoka katika uwekezaji ambao hugeuzwa mtaji na hivyo kutoa faida kubwa zaidi hapo baadae tofauti na uwekezaji wa muda maalum ambao faida inayopatikana inatokana tu na muda uliokaa ndani ya uwekezaji.

Je utajali ikiwa utapata riba ya asilimia 10 au 12 katika uwekezaji?

Ukweli ni kuwa, ukizingatia hilo utaweza kutengeneza tofauti kubwa katika ukuaji wa faida na mtaji kadiri muda unavyoenda/unavyoongezeka. Faida itokanayo na kompaundi inatokana na faida kuendelea kuongeza mtaji ambao huleta mapato makubwa kila mwaka. Mapato makubwa au faida kubwa au uwekezaji wa muda mrefu inaongeza kiasi cha mtaji kwa uwiano wa kijiometri.

**Matokeo ya Kompaundi.**

Kwa kutumia jedwali hapo chini, unaweza kuona matokeo ya nguvu ya kompaundi na faida zake kutokana na uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi 50,000/= na 5,000,000/= katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

**Jedwali Na. 07;**

| Riba | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka/Kiasi | 50,000/= | 5,000,000/= | 50,000/= | 5,000,000/= |
| 1 | 56,000.00 | 5,600,000.00 | 57,000.00 | 5,700,000.00 |
| 3 | 70,246.40 | 7,024,640.00 | 74,077.20 | 7,407,720.00 |
| 5 | 88,117.08 | 8,811,708.42 | 96,270.73 | 9,627,072.91 |
| 10 | 155,292.41 | 15,529,241.04 | 185,361.07 | 18,536,106.57 |
| 20 | 482,314.65 | 48,231,465.47 | 687,174.49 | 68,717,449.36 |

Jedwali namba 8, linaonesha matokeo ya nguvu ya kompaundi kutokana na faida zake kwa uwekezaji uliofanywa mara moja kwa kiasi cha shilingi milioni hamsini (50) na shilingi milioni mia moja (100) katika vipindi mbalimbali na kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

**Jedwali Na. 08;**

| Riba | 12% | | 14% | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka/ Kiasi** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** | **50,000,000/=** | **100,000,000/=** |
| 1 | 56,000,000.00 | 112,000,000.00 | 57,000,000.00 | 114,000,000.00 |
| 3 | 70,246,400.00 | 140,492,800.00 | 74,077,200.00 | 148,154,400.00 |
| 5 | 88,117,084.16 | 176,234,168.32 | 96,270,729.12 | 192,541,458.24 |
| 10 | 155,292,410.42 | 310,584,820.83 | 185,361,065.71 | 370,722,131.41 |
| 20 | 482,314,654.66 | 964,629,309.33 | 687,174,493.59 | 1,374,348,987.19 |

Nguvu ya kompaundi na faida yake inaoneshwa kwenye majedwali yafuatayo kwa mwekezaji anaewekeza kiasi cha shilingi 50,000/=, 100,000/=, 500,000/=, na shilingi milioni 1 kwa kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

**Jedwali Na. 09;** Uwekezaji wa shilingi 50,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

| Awamu za kuweka pesa | Riba / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 628,278.40 | 634,125.15 | 640,037.27 |
| 36 | 3 | 2,089,091.05 | 2,153,843.92 | 2,221,139.98 |
| 60 | 5 | 3,871,853.61 | 4,083,483.49 | 4,309,756.26 |
| 120 | 10 | 10,242,248.95 | 11,501,934.47 | 12,953,445.60 |
| 240 | 20 | 37,968,441.80 | 49,462,768.27 | 65,058,300.25 |

**Jedwali Na. 10;** Uwekezaji wa shilingi 100,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

| Awamu za kuweka pesa | Riba / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 1,256,556.81 | 1,268,250.30 | 1,280,074.54 |
| 36 | 3 | 4,178,182.11 | 4,307,687.84 | 4,442,279.95 |
| 60 | 5 | 7,743,707.22 | 8,166,966.99 | 8,619,512.51 |
| 120 | 10 | 20,484,497.89 | 23,003,868.95 | 25,906,891.21 |
| 240 | 20 | 75,936,883.60 | 98,925,536.54 | 130,116,600.51 |

FUND UKWASI Uhuru kwa mwekezaji

**Jedwali Na. 11;** Uwekezaji wa shilingi 500,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

| Awamu za kuweka pesa | Riba / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 6,282,784.05 | 6,341,251.51 | 6,400,372.68 |
| 36 | 3 | 20,890,910.55 | 21,538,439.18 | 22,211,399.75 |
| 60 | 5 | 38,718,536.09 | 40,834,834.93 | 43,097,562.55 |
| 120 | 10 | 102,422,489.45 | 115,019,344.73 | 129,534,456.05 |
| 240 | 20 | 379,684,417.99 | 494,627,682.69 | 650,583,002.53 |

**Jedwali Na. 12;** Uwekezaji wa shilingi 1,000,000/= kila mwezi kwa kutumia viwango tofauti vya riba.

| Awamu za kuweka pesa | Riba / Mwaka | 10% | 12% | 14% |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | 12,565,568.09 | 12,682,503.01 | 12,800,745.36 |
| 36 | 3 | 41,781,821.09 | 43,076,878.36 | 44,422,799.50 |
| 60 | 5 | 77,437,072.17 | 81,669,669.86 | 86,195,125.10 |
| 120 | 10 | 204,844,978.90 | 230,038,689.46 | 259,068,912.10 |
| 240 | 20 | 759,368,835.99 | 989,255,365.39 | 1,301,166,005.06 |

Kutokana na jedwali hapo juu, utagundua kuwa sio busara kupoteza muda na pesa kwa kuweka fedha zako kwenye uwekezaji usio na faida za kuridhisha kwa kipindi cha muda mrefu. Inabidi utambue kuwa, MUDA ni kigezo muhimu katika kufanya maajabu ya kompaundi.

Jambo la msingi la kujifunza:

(1) Wakati wote, tumia fursa zilizopo katika uwekezaji zenye kutoa faida kubwa ukilinganisha na uwekezaji mwingine

(2) Endelea kuwekeza kwa muda mrefu ili unufaike na maajabu ya kompaundi.

## 4.0 Mawasiliano

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mifuko yetu, tafadhali wasiliana nasi kwa anuani zifuatayo:

**Ofisi ya UTT DAR ES SALAAM**
Ofisi za UTT AMIS Dar es Salaam
Afisa Mtendaji Mkuu,
UTT AMIS Plc,
Ghorofa ya Pili, Jengo la Sukari, Mtaa wa Sokoine Drive na Ohio,
S.L.P 14825, Dar es Salaam
Simu Namba: +255 (0) 22 2128460
Namba za Bure: 0800112020
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz
Tovuti: www.uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MBEYA**
Ghorofa ya Pili, Jengo la NHIF, Mbeya
S.L.P 1210, Mbeya,
Simu Namba: +255 (0) 25 2500371
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MWANZA**
Mezzanine, Jengo la NSSF Commercial Complex
S.L.P 640, Mwanza,
Simu Namba: +255 (0) 28 2505072
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS DODOMA**
Ghorofa ya Sita, Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 1310, Dodoma
Simu Namba: +255 (0) 26 2323861
Nukushi: +255 26 2323862
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ARUSHA**
Ghorofa ya Nne, Jengo la Ngorongoro Conservation,
S.L.P 2490, Arusha,
Simu Namba: +255 (0) 27 2970625
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ZANZIBAR**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Sheikh Thabit Kombo- Michenzani
S.L.P 2190, Zanzibar
Simu Namba: +255 (0) 24 2941274
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

# Uhuru kwa mwekezaji

## Mifuko Mingine ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS

**Kwa maelezo zaidi kuhusu Mifuko yetu, tafadhali wasiliana nasi kwa anuani zifuatayo:**

**Ofisi ya UTT AMIS Dar es Salaam**
Afisa Mtendaji Mkuu, UTT AMIS Plc,
Ghorofa ya Pili, Jengo la Sukari, Mtaa wa
Sokoine Drive na Ohio,
S.L.P 14825, Dar es Salaam
Simu Namba: +255 (0) 22 2128460
Namba za Bure: 0800112020
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz
Tovuti: www.uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS DODOMA**
Ghorofa ya Sita, Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole,
S.L.P 1310, Dodoma
Simu Namba: +255 (0) 26 2323861
Nukushi: +255 26 2323862
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ARUSHA**
Ghorofa ya Nne, Jengo la Ngorongoro
Conservation,
S.L.P 2490, Arusha,
Simu Namba: +255 (0) 27 2970625
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MWANZA**
Mezzanine, Jengo la NSSF Commercial
Complex | S.L.P 640, Mwanza,
Simu Namba: +255 (0) 28 2505072
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS MBEYA**
Ghorofa ya Pili, Jengo la NHIF, Mbeya
S.L.P 1210, Mbeya,
Simu Namba: +255 (0) 25 2500371
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz

**Ofisi ya UTT AMIS ZANZIBAR**
Ghorofa ya Tatu, Jengo la Sheikh Thabit
Kombo- Michenzani | S.L.P 2190, Zanzibar
Simu Namba: +255 (0) 24 2941274
Nukushi: +255 (0) 22 2137593
Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz